Kiswahili

Kiongozi cha Mwalimu

Darasa la Tano


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 63

Jina la Chapisho: Kiswahili Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Tano

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9976 - 61 - 830 - 3

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Mwezi Oktoba Mwaka 20 18 kuwa Kiongozi cha Mwalimu, kwa ajili ya Darasa la Tano katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Kitabu cha Mwanafunzi cha Kiswahili Darasa la Tano, 2018.

Dkt. Edicome Cornel Shirima

Kaimu Kamishna wa Elimu.

Taasisi ya Elimu Tanzania

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 1 7/23/21 3:11 PM

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018
Chapa ya Pili 2021

ISBN: 978–9976–61–830–3

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 170 /+255 735 041 168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, wala kutafsiri kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 2 7/23/21 3:11 PM

Yaliyomo

Ukurasa

Utangulizi v

Shukurani xii

Sura ya Kwanza
Vitendawili 1

Sura ya Pili
Ngonjera 9

Sura ya Tatu
Nahau 19

Sura ya Nne
Kauli zetu 26

Sura ya Tano
Insha 33

Sura ya Sita
Kutambua nafsi 41

Sura ya Saba
Wanyama wafugwao 49

Sura ya Nane
Wanyama wa porini 55

Sura ya Tisa
Maua 62

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 3 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi
Shughuli za kila siku 69
Sura ya Kumi na Moja
Hali ya hewa 75
Sura ya Kumi na Mbili
Familia yetu 83
Sura ya Kumi na Tatu
Barua rasmi 90
Sura ya Kumi na Nne
Igizo 95
Sura ya Kumi na Tano
Shairi 103
Sura ya Kumi na Sita
Kuipenda nchi 110
Sura ya Kumi na Saba
Utenzi 115
Sura ya Kumi na Nane
Kupata taarifa muhimu 122
Sura ya Kumi na Tisa
Sifa za wanyama 133
Sura ya Ishirini
Miti yetu 140

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 4 7/23/21 3:11 PM

Utangulizi

Kiongozi hiki cha mwalimu wa Kiswahili Darasa la Tano ni mwendelezo wa kiongozi cha mwalimu wa somo la Kiswahili Darasa la Nne. Lengo kuu la kiongozi hiki ni kumpa mwalimu mbinu na maarifa ya kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la Tano. Katika kiwango hiki, mwanafunzi anatakiwa aweze kumudu vizuri stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika Kiswahili katika miktadha mbalimbali.

Lugha iliyotumika katika matini, msamiati, miundo, mazoezi ya lugha, methali, nahau na vitendawili ni ya kiwango cha juu kuliko ya Darasa la Nne. Mbinu mbalimbali za ufundishaji zimependekezwa. Una uhuru wa kubuni mbinu nyingine kulingana na mazingira, hali ya mahali, idadi na uwezo wa wanafunzi wako ili kuleta ufanisi katika ujifunzaji. Katika mchakato wote wa ufundishaji na ujifunzaji, washirikishe wanafunzi katika mazungumzo, kuimba, kuchora, kuigiza, kutamba na kughani.

Vifuatavyo ni vipengele muhimu ambavyo vitakusaidia mwalimu kufundisha stadi za lugha katika Darasa la Tano.

1. Msamiati

Ni jambo muhimu kuhakikisha kuwa, wanafunzi wanafahamu maneno yote mapya na kuyatumia katika sentensi. Misamiati ifundishwe kwa kutumia vitu halisi, picha na vielelezo, maelezo, vitendo, maigizo na maonesho. Kwa hiyo huna budi kutayarisha zana za kutosha za kufundishia na kujifunzia hasa zinazopatikana katika mazingira yako. Vidokezo vifuatavyo ni muhimu.

(a) Kutumia vitu halisi

Ni muhimu utumie vitu halisi katika kufundisha msamiati kwa kuwa wanafunzi wanapoona wanaelewa kwa urahisi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 5 7/23/21 3:11 PM

(b) ***Kutumia picha na vielelezo mbalimbali***

Iwapo utashindwa kupata vitu halisi, tumia picha na vielelezo. Picha na vielelezo vitayarishwe mapema na viwe vikubwa vya kutosha ili viweze kuonekana kwa urahisi kwa wanafunzi wote. Viwe na mvuto na uhalisia ili kueleza dhana kwa usahihi. Zingatia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mfano, tumia picha na vielelezo mguso ili kuwasaidia wanafunzi wasioona au wenye uoni hafifu.

(c) Kutumia vitendo

Inafaa maneno mengine hasa vitenzi na vivumishi yafundishwe kwa vitendo. Kwa mfano, chagua mwanafunzi na kumpa kifutio na kumwelekeza aende kufuta ubao. Mwanafunzi atafanya kama alivyoelekezwa. Uliza swali. _____ *(Taja jina la mwanafunzi*) alikuwa anafanya nini? Pokea majibu na kisha eleza kuwa ulikuwa unafundisha neno "futa".

2. Miundo

Muundo ni mpangilio wa maneno na uhusiano wake katika sentensi. Katika muundo mmoja inawezekana kutunga sentensi kadhaa zenye maana tofauti.

Katika kitabu cha mwanafunzi alama za **kistari** (yaani ____) na **dotidoti** (yaani……..) zinatumika kuonesha nafasi ya kujaza miundo iliyolengwa. Alama ya kistari huonesha kuwa neno halijakamilika. Alama ya dotidoti huonesha kuwa neno au maneno hayapo. Katika miundo, nafasi hizo zinatakiwa zijazwe. Nafasi ya kistari itajazwa na sehemu ya neno na dotidoti itajazwa kwa neno au maneno. Waongoze wanafunzi kujaza nafasi hizo. Kwa mfano:

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 6 7/23/21 3:11 PM

(a) Muundo
"**ana**____" unaweza kujazwa na kuwa: ***ana****lima*, ***ana****soma*, ***ana****imba*, ***ana****tembea* na kuendelea.

(b) Muundo
"...**ata**__" unaweza kujazwa ukawa *Bibi* ***ata****kuja*.

Miundo ifundishwe kwa lugha rahisi na inayoeleweka. Irudiwerudiwe ili wanafunzi waizoee na kujenga kumbukumbu. Sentensi zinazotungwa kusisitiza miundo lazima zilingane na mazingira na maisha ya wanafunzi ili waweze kuzitumia katika maisha yao ya kila siku. Andaa mazoezi ya ziada kutokana na misingi ya sura husika.

3. Methali

Methali zifundishwe kadiri zinavyotokea katika hadithi au zijengewe maelezo yanayohusiana na mazingira zinamotumika. Eleza methali kwa kutumia masimulizi yanayohusiana na maisha ya kila siku. Ili wanafunzi wagundue maana za methali hizo, unaweza kufundisha methali zinazofanana au zilizo kinyume na zile zilizomo katika hadithi. Ufundishaji wa methali bila kuzihusisha na mazingira ya maisha haufai. Wanafunzi waelekezwe kutoa mianzo au miisho ya methali zao na wengine wamalizie. Pia, wanafunzi waongozwe kutumia methali katika miktadha mbalimbali.

4. Vitendawili

Fundisha vitendawili kwa kuwapa wanafunzi nafasi ya kutega na kutegua vitendawili vyao. Waelekeze kupeana mji kila wanaposhindwa kupata jibu sahihi. Uhusiano uliopo kati ya kitendawili na jibu lake ujadiliwe. Vitendawili pia vinaweza kutumiwa kama chemshabongo mwanzo wa somo la Kiswahili. Vitendawili vipya vyenye mantiki vikubaliwe. Kumbuka kwamba vitendawili hutofautiana kulingana na mazingira.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 7 7/23/21 3:11 PM

5. Misemo na nahau

Fundisha misemo na nahau kwa maelezo, picha, matendo, vitu halisi na majadiliano. Waongoze wanafunzi jinsi ya kutumia misemo na nahau hizo katika sentensi. Kwa mfano, maneno yako **yalimkata maini** (Maneno yako yalimuudhi kupindukia).

6. Ufahamu

Lengo la kusoma ni kuelewa kilichoandikwa, yaani ufahamu. Ziko njia mbalimbali za kufundishia kusoma. Unashauriwa kufuata mwongozo uliotolewa katika kitabu hiki. Hata hivyo, uwe tayari kubadili njia iwapo utapata vikwazo, kwani ufanisi wa mwanafunzi ndio lengo letu. Zifuatazo ni njia mbalimbali za kusoma:

(a) Kusoma kimya

Katika somo la kusoma kimya waelekeze wanafunzi kusoma kimya bila kufungua mdomo. Wanafunzi wasome sura yote na kujibu maswali ya ufahamu. Licha ya maswali yaliyomo kitabuni, tunga maswali mengine ya nyongeza kuhusiana na sura husika.

(b) Kusoma kwa sauti

Lengo la kusoma kwa sauti ni kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa lafudhi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia sauti ya kutosha, matamshi, shadda, kiimbo, matumizi ya alama za uandishi kwa usahihi na hisia. Katika somo la kusoma kwa sauti onesha mfano wa usomaji mzuri. Pia, teua wanafunzi wengi kadiri iwezekanavyo kusoma kwa sauti. Hii itategemea muda, idadi na kiwango cha usomaji wa wanafunzi.

(c) Kusoma kwa ziada

Lengo la kusoma kwa ziada ni kumwezesha mwanafunzi kusoma kwa ufahamu na kwa kasi stahiki na kumwongezea maarifa. Kusoma kwa ziada pia humjengea mwanafunzi tabia ya kupenda kujisomea. Ongoza usomaji huu. Yafuatayo yazingatiwe kutekeleza jambo hili:

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 8 7/23/21 3:11 PM

(i) Waelekeze sura ya kusoma katika kipindi hicho.

(ii) Wanafunzi wasome kimya.

(iii) Waulize maswali. Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa kusema au kwa kuandika. Waongoze wanafunzi kutoa muhtasari wa habari waliyoisoma.

(iv) Katika baadhi ya vipindi, badala ya kujibu maswali, wanafunzi waelekezwe kuchora, kusimulia, kuigiza au kuimba ili kusisitiza maarifa waliyoyapata.

(v) Inafaa somo la kusoma kwa ziada lifanyike mara moja ndani ya wiki mbili.

7. Mazoezi ya lugha

Katika kitabu hiki yamo mazoezi mbalimbali ya lugha kwa kila sura. Mazoezi hayo hujumuisha uchaguzi wa jibu sahihi, kujaza nafasi, kueleza maana za maneno, kuunganisha sehemu mbili za sentensi, umoja na wingi, kubadili nyakati na mengineyo. Fundisha zoezi moja au mawili ya lugha kwa kipindi kimoja na kuongeza mazoezi kulingana na mazingira na uwezo wa wanafunzi.

8. Utungaji

Sehemu kubwa ya mazoezi ya utungaji katika darasa hili ni ya kuongozwa. Uongozi huo umefanywa kwa:

(a) Kuchagua na kupanga sentensi zilizochanganyika, hasa zilizotokana na habari iliyosomwa au kuzungumzwa.

(b) Kutumia picha. Wanafunzi wanaweza kuchora, kama wataelekezwa na mwalimu kufanya hivyo. Wanaweza pia kuchorewa picha zinazohusu habari fulani. Wanafunzi wanatakiwa kutoa maelezo kuhusu picha moja au zaidi zilizotolewa.

(c) Kukamilisha habari.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 9 7/23/21 3:11 PM

(d) Kusimulia na kuelezea hadithi au habari mbalimbali. Wanafunzi wahimizwe kuigiza, kuimba, kutenda na kuitikia.

(e) Kuuliza maswali ambayo majibu yake yataunda hadithi.

Toa uzito sawa wa mazoezi ya utungaji wa mdomo na wa kuandika. Hii itawasaidia wanafunzi kukuza uwezo wa kujieleza kwa mdomo na kwa maandishi.

9. Ushairi

Ushairi ni uwanja mwingine wa fasihi. Katika kiwango hiki mwanafunzi asome na kuimba mashairi na ngonjera. Pia, atambue vina, mizani, mishororo na urari katika mashairi. Vilevile aelewe mawazo makuu na ujumbe uliomo katika shairi.

10. Mwandiko

Kazi ya kufundisha mwandiko iliyoanza Darasa la Kwanza iendelezwe na kuimarishwa katika darasa hili. Sisitiza uumbaji mzuri wa herufi, hati ya kuunga, ukataji wa maneno kwa kuzingatia silabi na nafasi kati ya neno na neno. Pia, alama za uandishi zisisitizwe. Sisitiza usahihi wa mwandiko katika kila somo linalohusisha kuandika.

11. Imla

Ni somo ambalo wanafunzi hupimwa uwezo wa kusikiliza na kuandika kwa usahihi kile walichosomewa na mwalimu. Wanafunzi wengi hawawezi kuandika habari vizuri kwa kufuata taratibu na alama za uandishi. Vilevile, hawawezi kuandika kwa kasi kwa kufuata msomaji anavyosoma. Fundisha uandishi wa imla kwa kuzingatia kanuni.

12. Matayarisho / maandalizi ya somo

Soma kitabu cha mwanafunzi na kiongozi cha mwalimu kwa makini na kukielewa kabla ya kufundisha. Hii itakusaidia kuelewa kwa undani

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 10 7/23/21 3:11 PM

vipengele vyote unavyotakiwa kufundisha. Hakikisha unaandaa somo lako vizuri kama inavyotakiwa.

13. Fikiri

Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyoorodheshwa katika kipengele cha *fikiri* katika kila sura kabla ya kusoma. Maswali hayo yatakusaidia kupata maarifa ya awali aliyonayo mwanafunzi kuhusu sura husika.

14. Mgawanyo wa vipindi

Katika mwaka wa masomo kutakuwa na siku 194 ambazo ni sawa na wiki 39 za masomo. Makadirio ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Katika darasa hili kuna vipindi 7 vya Kiswahili kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

15. Mrejesho kwa wanafunzi

Sahihisha kazi zote za wanafunzi na kuwapa mrejesho. Ni vema kufanya masahihisho darasani ili kila mwanafunzi atambue kosa lake na kujisahihisha.

Shukurani

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 11 7/23/21 3:11 PM

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kiongozi hiki cha mwalimu.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

Waandishi: Rose S. Chipindula, Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Dkt. Adventina A. Buberwa, Dkt. Mgogo Yangson, Agnes S. Maguga, Faraja J. Mwendamseke, Winifrida J. Mutagwaba, Ester K. Koroti, Marko M. Julius na Oscar A. Ndalibamale.

Wahariri: Mussa R. Kaoneka (BAKITA), Luinasia E. Kombe (Mwenyekiti wa jopo) na Jopo la wahariri

Msanifu: Janeth E. Mbwiga

Wachoraji: Alama Art and Media Production Limited

Mratibu: Rose S. Chipindula

Pia, TET inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki.

Aidha,Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi na kugharamia kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 12 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kwanza

Vitendawili

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kutega na kutegua vitendawili. Pia, atajifunza kuvihusisha vitendawili hivyo na vitu vilivyomo katika mazingira yanayomzunguka kwa usahihi. Vilevile, atajifunza misamiati, nahau, methali, ukanushi, utungaji na kufanya mazoezi mengine ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma habari ya **Mtego wa vitendawili**

(b) Kueleza maana ya kitendawili

(c) Kutega na kutegua vitendawili

(d) Kuhusianisha vitendawili na vitu vilivyomo katika mazingira

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati za vitendawili, kalamu rashasha, bangokitita na diski ya vitendawili (sidii ya vitendawili)

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo ukurasa wa kwanza kwenye kipengele cha *fikiri* katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Mtego wa vitendawili**, iliyopo katika ukurasa wa kwanza hadi wa tatu katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 1 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Taja majina ya wanyama uliowasoma katika habari.

(ii) Ni vitendawili gani ambavyo umevisoma kwenye habari?

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 4 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza nini unatarajia kifanyike katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmoja mmoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na kuzirekebisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 2 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *ghala, jibanza, gutuka, hila, mbwembwe, dhihaka, mikogo, kiinimacho* na *madaha* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na waongoze kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Kagua usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 la ukurasa wa 4 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu na maana zake, kwa mfano:

Nahau	**Maana**
piga chenga	kwepa
piga domo	ongea sana
tia moyo	kumpa mtu matumaini
mezea mate	tamani sana

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 5 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 3 7/23/21 3:11 PM

Majibu : *1. weza/ mudu jambo* *2. kutembea kwa miguu*
3. poteza matumaini *4. fikiri sana*
5. kupanga mipango ya siri

Somo la 5: Misemo

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja misemo mbalimbali wanayoifahamu.

(b) Waongoze wanafunzi kufafanua na kutoa maana ya misemo.

Mfano : *Lowa chapachapa*

Lowa maji kabisa

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 5 wa kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *1. miaka mingi*
2. utu uzima ni busara/suluhu ya matatizo
3. sumbua

Somo la 6: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu

Mfano: *Kitendawili – Tega*

Bibi hatui mzigo wake – <u>Konokono au kobe</u>

Endapo mwanafunzi hatatoa jibu sahihi, mtegaji apewe mji ili atoe jibu sahihi.

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia maelezo, picha, na mifano kutega na kutegua vitendawili. Unaweza kutumia shairi kutega kitendawili, kwa mfano:

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 4 7/23/21 3:11 PM

Kuku wangu wa ajabu, anatetea jioni,

Yai kwake ni adimu, natafuta silioni,

Nilizipiga hesabu, nikasaka vichakani,

Megundua kuku wangu, anatagia mibani.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A na B lililopo ukurasa wa 5 na 6 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: 5 A. *(i) ndege (ii) mbarika (iii) firigisi (iv)mahindi (v) kinyonga (vi)mafiga (vii) ugali (viii) usingizi (ix) utelezi (x) miguu/nyayo/kutembea*

5 B. *(i) Ukoo wangu hauishiwi safari.*
(ii) Napigwa faini kosa silijui.
(iii) Amefika kabla mjumbe hajarudi.
(iv) Rafiki kutoka mbali na mkono wake kiunoni.
(v) Afahamu kuchora lakini hajui achoracho.
(vi) Yakija masika hawalali.

Somo la 7: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Toa mfano uliopo katika zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 7 katika kitabu cha mwanafunzi. Ongeza mifano mingine.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 7 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *1. hukosa yote* *2. Mtaka cha uvunguni*
3. Hakuna marefu *4. ndiye rafiki wa kweli*
5. yasiyokuwa na mbu *6. ni arobaini*
7. Ujanja mwingi

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 5 7/23/21 3:11 PM

Somo la 8: Mazoezi ya lugha

A. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 7 A lililopo ukurasa wa 7 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 A lililopo ukurasa wa 7 katika kitabu cha mwanafunzi.

B. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu zoezi litakalofanyika.

(ii) Toa mifano ya maswali yenye majibu ya KWELI na SI KWELI.

Mfano : Mzee Ngedere ana pembembili. *SI KWELI*
Nyuki hutengeneza asali. *KWELI*

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 B ukurasa wa 8 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *(i) SI KWELI (ii) SI KWELI (iii) KWELI*
(iv) KWELI (v) SI KWELI (vi) KWELI
(vii) KWELI (viii) KWELI

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 6 7/23/21 3:11 PM

Somo la 9: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo hili. Sisitiza watakapoandika waandike imla hiyo kwa hati ya wima ya kuunga. Pia, wazingatie alama za uandishi.

(b) Wasomee wanafunzi imla ifuatayo kwa kasi ya kawaida. Wanafunzi wasikilize bila kuandika.

Walibembelezwa kwa hila wakakubali kuingia ndani. Wakawekwa kwenye chumba kilichopambwa vizuri. Humo paliandaliwa vyakula vinono. Wakala na kunywa kwa furaha huku wakipeana michapo. Siku za mwizi ni arobaini, na ujanja mwingi mbele kiza. Lo! Walipogutuka wakajikuta wamekwishafungiwa humo. Nje ya chumba hicho alikuwepo binadamu akicheka kwa dharau. Wakadhani ni kiinimacho. Kumbe Ngedere alikuwa amekula njama kuwakamata kwa hila na hilo lilikuwa gereza la waharibifu wa mazao. Majuto ni mjukuu.

(c) Wasomee tena mara ya pili kwa kufuata vituo na alama za uandishi huku wakiandika kwenye madaftari yao.

(d) Wasomee taratibu huku wao wakifuatisha na kuhakiki kile walichokiandika.

(e) Sahihisha kazi kwa kuzingatia uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, matumizi ya alama za uandishi, matumizi ya herufi kubwa, hati ya wima ya kuunga na usafi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 7 7/23/21 3:11 PM

Somo la 10: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Ongoza majadiliano kuhusu uhusiano uliopo kati ya vitendawili na vitu vilivyopo katika mazingira ya mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 8 lililopo ukurasa wa 8 katika kitabu cha mwanafunzi kwa kuzingatia maelekezo.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi, mtiririko wa mawazo, na matumizi ya vitendawili.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 8 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Pili

Ngonjera

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atasoma na kujifunza namna ya kutamba ngonjera kwa kuzingatia kanuni za utambaji. Pia, atataja wahusika katika ngonjera na kutunga beti mbili au zaidi za ngonjera. Vilevile, ataeleza umuhimu wa ngonjera na kufanya mazoezi mbalimbali ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma ngonjera inayohusu kipindupindu

(b) Kutamba ngonjera kwa sauti ya utambaji

(c) Kubaini wahusika waliomo katika ngonjera

(d) Kueleza umuhimu wa ngonjera

(e) Kutunga ngonjera

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), bangokitita na kalamu rashasha.

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 9 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya ngonjera kuhusu kipindupindu iliyopo ukurasa wa 9 - 11 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 9 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Ngonjera uliyoisoma inahusu janga gani ?

(ii) Kwa nini watu walishauriwa kwamba wadumishe usafi?

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie ngonjera waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 12 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu ngonjera ya **Kipindupindu**. Kisha wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu za kusoma ngonjera kwa sauti.

(b) Chagua wahusika Hekima na Bahati na kuwapa uhusika katika kusoma ngonjera.

(c) Toa muda mfupi kwa kila mhusika kusoma sehemu yake.

(d) Waongoze wanafunzi wasome ngonjera kwa kuzingatia uhusika na kanuni za kusoma kwa sauti. Wanaweza kusoma ngonjera hii zaidi ya mara moja.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera kwa usahihi. Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wagawe wanafunzi katika makundi mawili, yaani upande wa Bahati na upande wa Hekima, ili wanafunzi wengi waweze kusoma.

(h) Wanafunzi warudie kutamba ngonjera kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 10 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *kipindupindu, viporo, janga, dhoofika, madhila, soni, kiri, teta*, *uchochoro* na *abadani.*

(b) Andika maneno hayo ubaoni kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya kila neno.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

Mfano: *Pili hana raha kwa sababu madhila yamemsonga.*

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 12 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao. Sentensi ziwe tofauti na zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 13 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni. Tumia mifano iliyopo zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 13 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 13 katika kitabu cha mwanafunzi kwa mazungumzo, kisha andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 13 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao. Sentensi ziwe tofauti na sentensi zilizotolewa mfano.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 11 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu nahau. Waulize wanafunzi wataje nahau wanazozifahamu.

(b) Tumia mfano uliopo zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 13 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 ukurasa wa 13 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 6: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu. Wakumbushe kumpa mji yule aliyetega kitendawili kikawashinda kujibu.

Mfano : *Napigwa faini kosa silijui. – <u>kujikwaa</u>*
Wakikua mama yao huwatupa mbali kwa kishindo. – <u>mbarika</u>

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia maelezo, picha, na mifano kutega na kutegua vitendawili.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 14 – 15 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 7: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kukamilisha methali.

Mfano: ……. haina baraka.

<u>*Haraka haraka*</u> haina baraka.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 12 7/23/21 3:11 PM

Vita vya panzi.....

Vita vya panzi *furaha ya kunguru.*

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa 15 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *1.hafaidi hadi siku ya Idi* *2. Shukurani ya punda*
3. kwa binadamu mchungu *4. Samaki mkunje*
5. si ujinga

Somo la 8: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika maneno kwa kirefu

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia mfano uliopo zoezi la 7 A lililopo ukurasa wa 15 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi warejee ngonjera iliyopo ukurasa wa 9 -11 katika kitabu cha mwanafunzi ili wabaini maneno yaliyoandikwa kwa kifupi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 A lililopo ukurasa wa 15 katika kitabu cha mwanafunzi.

B. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu kinyume cha maneno.

(ii) Waongoze wanafunzi kutoa kinyume cha maneno yafuatayo:

dogo - kubwa

rafiki - adui

nene - nyembamba

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 13 7/23/21 3:11 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 B ukurasa wa 16 katika kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu : *(i) nawiri (ii) joto (iii) raha (iv) patana*
(v) kana (vi) lia (vii) uongo (viii) zama (ix) nuru

C. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutoa mfano wa sentensi kujibu **KWELI** au **SI KWELI.** Unaweza kutumia sentensi ya kwanza au ya pili katika zoezi la 7 C ukurasa wa 16 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Ongeza sentensi nyingine kuimarisha zoezi hili.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 C lililopo ukurasa wa 16 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu: *(i) SI KWELI (ii) KWELI (iii) KWELI*
(iv) SI KWELI (v) SI KWELI (vi) KWELI
(vii) KWELI (viii) KWELI

D. Kubadili sentensi ziwe katika wakati uliopita

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo. Tumia mfano uliotolewa katika zoezi la 7 D ukurasa wa 17 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi zilizo katika wakati uliopo na ujao. Ziandike sentensi hizo ubaoni.

(iii) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi hizo kuwa katika wakati uliopita.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 D lililopo ukurasa wa 17 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 14 7/23/21 3:11 PM

E. Kuchagua jibu lililo sahihi na kuandika herufi yake katika kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano kwa kuandika swali ubaoni ili wanafunzi wachague jibu lililo sahihi.

Mfano: Nani alitoa ujumbe kuhusu madhara ya kipindupindu ?

(a) Bahati

(b) Hekima

(c) wote wawili

(d) hakuna.

b

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 E lililopo ukurasa wa 17 - 18 katika kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu: *(i) c (ii) b (iii) a (iv) d (v) c (vi) c*

F. Kukamilisha maneno ya sehemu B ili yakubaliane na sehemu A

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo jinsi ya kufanya zoezi la kukamilisha maneno ya sehemu B ili yakubaliane na ya sehemu A. Tumia mfano uliopo katika zoezi la 7 F katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 F lililopo ukurasa wa 19 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 15 7/23/21 3:11 PM

G. Kuandika maneno yenye maana sawa na maneno yaliyotolewa

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno wanayoyafahamu yenye maana sawa . Tumia mfano uliopo zoezi la 7 G lililopo ukurasa wa 19 katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 G lililopo ukurasa wa 19 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) dagaa (ii) pesa au hela (iii) fimbo au mkwaju (iv) garimoshi (v) binti (vi) mtoto (vii) chooni (viii) asilani/sini/kamwe/katu*

Somo la 8: Utungaji

A. Kukamilisha habari kwa kujaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo jinsi ya kukamilisha habari kwa kujaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia majibu sahihi ili kukamilisha utungaji.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyomo kwenye kisanduku ukurasa wa 20 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 8 A lililopo ukurasa wa 20 katika kitabu cha mwanafunzi kwa kuandika kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) wanaoga	*(ii) machafu*	*(iii) ilijaa*
(iv) kutambua	*(v) akawaona*	*(vi) wadudu*
(vii) wakavaa	*(viii) akawaambia*	*(ix) kichocho*
(x) waliondoka	*(xi) aliondoka*	

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 16 7/23/21 3:11 PM

(iv) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi na mwandiko mzuri.

(v) Baada ya kusahihisha, chagua kazi iliyoandikwa vizuri; wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

B. Kutunga ngonjera yenye beti mbili kuhusu nzi

Hatua za Ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera ya kipindupindu iliyoko ukurasa wa 9 - 11 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Chagua wahusika wawiliwawili wasome kwa kupokezana na kutamba beti kwa zamu.

(iii) Wakumbushe wanafunzi kuwa ngonjera ni mashairi ya kujibizana watu wawili au vikundi kwa kuzingatia urari wa vina, mizani na vituo.

(iv) Waelekeze kutunga ngonjera kuhusu nzi.

(v) Waongoze wanafunzi wataje umbo, tabia, sifa na mahali anapoishi nzi. Kisha andika ubaoni kadiri wanavyotaja.

(vi) Waongoze wanafunzi kuunda maneno yenye silabi za mwisho zinazofanana kutokana na maneno yale yaliyoko ubaoni.

Mfano: *shimoni, jalalani, gizani, ndani, jikoni na pembezoni.*

(vii) Waongoze kutunga sentensi fupi zenye silabi nane, kisha waweke alama ya mkato mwisho wa sentensi hizo.

(viii) Wajaribu kuunda maneno yanayoishia na silabi zinazofanana kutengeneza vina vya kati na vya mwisho, sentensi nne nne kutengeneza ubeti.

(ix) Waongoze wanafunzi kutafuta vina vya kati na vya mwisho katika sentensi. Wakumbushe kuwa idadi ya silabi katika sentensi ni 16. Waandike beti mbili.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 17 7/23/21 3:11 PM

(x) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 8 B lililopo ukurasa wa 20 katika kitabu cha mwanafunzi.

(xi) Sahihisha kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uandishi wa ngonjera.

(xii) Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera walizozitunga.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 18 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Tatu

Nahau

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kutumia nahau katika habari fupi na kuelezea maana zake pamoja na umuhimu wake. Pia, atajifunza kutafsiri taswira inayoakisiwa na nahau. Vilevile, atajifunza misamiati, miundo, ukanushi, mazoezi mengine ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma hadithi kuhusu ***Jongoo na nyoka***

(b) Kutaja nahau wanazozifahamu

(c) Kutumia nahau katika habari fupi

(d) Kueleza maana za nahau

(e) Kueleza umuhimu wa nahau

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya nahau, kalamu rashasha, bangokitita na diski ya nahau

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 21 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi ya **Jongoo na nyoka**, iliyopo ukurasa wa 22 - 23 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 19 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Hapo zamani jongoo alikuwa na maumbile gani?

(ii) Nyumbani kwa mwewe kulitokea nini?

(d) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa 22 katika kitabu cha mwanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 ukurasa wa 24 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmoja mmoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 20 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *kwaa, fariji, ahueni, tibu, matibabu, shawishi* na *meremeta* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 ukurasa wa 24 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazozitunga hazifanani na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa 24 - 25 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni.

(d) Waelekeze wanafunzi kanuni za miundo ya "…..**japokuwa**….." na "**Kama hutajali**……..."

(e) Toa mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa 24 - 25 katika kitabu cha mwanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na andika sentensi hizo ubaoni.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 21 7/23/21 3:11 PM

(g) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(h) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 24 - 25 katika kitabu cha mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau zilizotumika katika habari ya Jongoo na nyoka ukurasa wa 22 - 23 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Andika nahau walizozitaja wanafunzi ubaoni.

(c) Angalia usahihi wa nahau zilizotajwa na wanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya nahau hizo kwa kutoa mfano.

Mfano: *bega kwa bega – kushirikiana, kwa pamoja.*

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 ukurasa wa 25 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika umoja na wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia mfano uliopo zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 25 katika kitabu cha mwanafunzi kuwaelekeza dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 25 - 26 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 22 7/23/21 3:11 PM

B. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 5 B ukurasa wa 26 katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

Mfano: *Mwalimu alichelewa kuingia darasani*

Mwalimu <u>hakuchelewa</u> kuingia darasani.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B ukurasa wa 26 katika kitabu cha mwanafunzi.

C. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 26 katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuongeza mfano.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 26 - 27 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

majibu: *(i) zibua taratibu (ii) pona (iii) kataa (iv) polepole/ (v) rudi (vi) ubaya (vii) woga (viii) mkaidi*

D. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya maswali yenye majibu ya KWELI na SI KWELI.

Mfano: *Hapo zamani nyoka alikuwa na macho pamoja na miguu. SI KWELI*

Nahau zina maana. KWELI

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 23 7/23/21 3:11 PM

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 27 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) SI KWELI (ii) SI KWELI (iii) KWELI (iv) KWELI (v) KWELI (vi) SI KWELI (vii) KWELI (viii) KWELI*

E. Kuandika sentensi katika wakati uliopo

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi katika wakati uliopo.

(ii) Andika ubaoni sentensi zilizotungwa na wanafunzi.

(iii) Angalia usahihi wa sentensi zilizotungwa.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E ukurasa wa 27 katika kitabu cha mwanafunzi.

F. Kutunga sentensi kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo katika zoezi la 5 F ukurasa wa 28 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyomo kwenye jedwali.

(iii) Waongoze kutunga sentensi tatu kutokana na jedwali kwa mazungumzo.

(iv) Angalia usahihi wa sentensi zilizotungwa.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa 28 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 24 7/23/21 3:11 PM

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo jinsi ya kuandika habari katika mtiririko mzuri.

(b) Nakili ubaoni mwanzo wa habari iliyopo ukurasa wa 28 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma mwanzo wa habari iliyoandikwa ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kumalizia habari kwa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika zoezi la 6 ukurasa wa 28 katika kitabu cha mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia, alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, matumizi sahihi ya herufi kubwa na matumizi sahihi ya nahau walizopewa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 25 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Nne

Kauli zetu

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kauli halisi na kauli taarifa. Pia, atajifunza kutunga sentensi kwa kutumia kauli hizo. Vilevile, atajifunza misamiati, miundo, nahau, ukanushi, kisha atafanya mazoezi mbalimbali ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma habari ya **Fabu apata zawadi**

(b) Kutunga sentensi kwa kutumia kauli halisi

(c) Kutunga sentensi kwa kutumia kauli taarifa

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), bangokitita na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 29 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Fabu apata zawadi** iliyopo ukurasa wa 29 - 31 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Bera anasoma darasa la ngapi?

(ii) Kwa nini wanafunzi walimshangilia Fabu?

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 26 7/23/21 3:11 PM

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 ukurasa wa 31 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na kurekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *bingwa, heshimu, azimia, sumbua, adhabu, adabu, usia, nderemo* na *vifijo* kwa kutumia mbinu ya maelekezo, vitu halisi, picha, na maigizo.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 27 7/23/21 3:11 PM

(b) Andika maneno hayo ubaoni kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Kisha andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 32 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu miundo.

(b) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia mifano iliyopo katika zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 32 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Nakili miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 32 katika kitabu cha mwanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma miundo ubaoni.

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na kuandika sentensi hizo ubaoni.

(f) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 32 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 28 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu.

(b) Nakili ubaoni zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 32 - 33 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia mfano uliopo kwenye zoezi la 4 ukurasa wa 32 katika kitabu cha mwanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 32 - 33 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu: *1. ongeza bidii 2. tembea 3. poteza matumaini 4. kunywa pombe 5. kata tamaa.*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kubadili kauli halisi kuwa kauli taarifa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu kauli halisi na kauli taarifa.

(ii) Waongoze wanafunzi kubadili kauli halisi kuwa kauli taarifa kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi 5 A ukurasa wa 33 katika kitabu cha mwanafunzi. Waweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 33 katika kitabu cha mwanafunzi.

B. Kubadili kauli taarifa kuwa kauli halisi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 5 B ukurasa wa 33 katika kitabu cha mwanafunzi. Pia, ongeza mifano mingine.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 29 7/23/21 3:11 PM

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B ukurasa wa 33 katika kitabu cha mwanafunzi.

C. Kuandika kauli halisi nne (4) na kauli taarifa nne (4) kutokana na habari waliyoisoma

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Tumia mifano ya kauli halisi na kauli taarifa iliyopo katika habari ya **Fabu apata zawadi.**

Mfano: *Fabu alijibu kwa upole, "Samahani kama nimewaudhi."*
– Kauli halisi
Aliazimia moyoni kwamba siku moja atawauliza wenzake kwa nini walikuwa wakichelewa shuleni.
– Kauli taarifa

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa 34 katika kitabu cha mwanafunzi.

D. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi namna ya kukanusha sentensi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 34 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 34 katika kitabu cha mwanafunzi.

E. Kubadili sentensi kuwa katika umoja

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Waongoze wanafunzi kujadili dhana ya wingi na umoja kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa 34 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 30 7/23/21 3:11 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa 34 katika kitabu cha mwanafunzi.

F. Kutunga sentensi kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo zoezi la 5 F ukurasa wa 35 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Toa mifano kwa kutunga sentensi kutokana na jedwali.

Mfano: *Mwalimu aliusia kwamba ni muhimu kusoma kwa bidii.*

Raja alisema kuwa Jumatano ni siku ya usafi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa 35 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 7: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya na nafasi kati ya neno na neno na matumizi ya herufi kubwa.

(b) Soma kwa sauti kifungu cha habari huku wanafunzi wakisikiliza.

Siku moja Nyakabi aliwatembelea wazazi wake. Akiwa njiani alikutana na wadogo zake. Nyakabi na wadogo zake walielekea nyumbani. Walipofika Kandida akasema, "Tulikuwa tunakuja kwako." Nyakabi alimtazama Kandida kisha akauliza, "Mmekuja kuchukua nguo zenu?" Kandida akasema kwa sauti ya furaha, "Hapana."

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 31 7/23/21 3:11 PM

(c) Soma tena hatua kwa hatua huku wanafunzi wakiandika kwenye madaftari yao.

(d) Soma kifungu chote ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hazijasahihishwa.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, hati ya wima ya kuunga, matumizi ya herufi kubwa, na usafi wa kazi.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo jinsi ya kumalizia habari katika mtiririko mzuri.

(b) Waongoze wanafunzi kwa kuwaandikia ubaoni mambo ya kuzingatia kama yalivyoandikwa katika zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 35 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 35 katika kitabu cha mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 32 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Tano

Insha

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu maana na hatua za uandishi wa insha na muundo wake. Vilevile, atajifunza msamiati, methali, nahau na kufanya mazoezi mbalimbali ya lugha. Pia ataweza kuandika insha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma insha

(b) Kueleza maana ya insha

(c) Kueleza hatua za uandishi wa insha

(d) Kueleza muundo wa insha

(e) Kuandika insha

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya muundo wa insha, bangokitita na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 36 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Toa maelezo mafupi kuhusu somo utakalofundisha.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya insha ya **Maisha ya Kanenge**, iliyopo ukurasa wa 36 - 39 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 33 7/23/21 3:11 PM

(d) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:

(i) Kanenge alianza kuishi na shangazi yake akiwa na umri gani?

(ii) Shangazi alimpatia Kanenge vidonge vingapi?

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 39 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza nini unatarajia kifanyike katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmoja mmoja kwa zamu, bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 34 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *yatima, nasaha, athirika, ridhaa, tafakari* na *virusi* kwa kutumia maelezo, picha, mazingira halisi na matendo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 39 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi wataje nahau wanazozifahamu.

(b) Andika nahau hizo ubaoni, kisha wanafunzi wazisome na kutoa maana zake.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia nahau hizo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 40 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha wanafunzi hawatumii sentensi zilizotolewa mfano.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 35 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Waongoze kukamilisha methali kwa kutumia mifano ifuatayo:

Samaki mkunje .....

Samaki mkunje <u>angali mbichi</u>.

....., mauti nyuma.

<u>Tamaa mbele</u>, mauti nyuma.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 40 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *1. Damu 2. tugange yajayo 3. mngoje chini*

4. Mwenda kwao 5. haulambwi

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuonesha sentensi zenye kauli halisi na kauli taarifa

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 A uliopo ukurasa wa 40 katika kitabu cha mwanafunzi kuonesha sentensi zenye kauli halisi na kauli taarifa. Ongeza mifano mingine ya kauli halisi na kauli taarifa.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 40 - 41 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *(i) kauli taarifa (ii) kauli halisi (iii) kauli taarifa*
(iv) kauli halisi (v) kauli taarifa (vi) kauli taarifa
(vii) kauli halisi (viii) kauli halisi
(ix) kauli taarifa (x) kauli halisi

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 36 7/23/21 3:11 PM

B. Kuweka herufi kubwa mahali panapostahili

Hatua za ufundishaji

(i) Andika sentensi mbili ubaoni bila kuzingatia matumizi ya alama ya herufi kubwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kuweka herufi kubwa katika maneno yanayounda sentensi hizo.

Mfano: *kakeno amekimbilia upande wa kusini.*

<u>K</u>akeno amekimbilia upande wa <u>K</u>usini.

pira na chonanga wamekwenda shambani.

<u>P</u>ira na <u>C</u>honanga wamekwenda shambani.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa 41 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) Baba...Ashura (ii)Hazole...Dodoma*
(iii)Njalambaya... (iv) Ameelekea...Kaskazini
(v) Mwalimu...Chuo...Ualimu...Butiama
(vi)Mimi...Butimba (vii) Mto Rufiji...
(viii) Seni...Jumamosi (ix) Serengeti .....
(x) Shule...Novemba

C. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Toa mifano ya kinyume cha maneno

Mfano: *nyuma – mbele*

shika – achia

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 41 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 37 7/23/21 3:11 PM

Majibu: *(i) binti (ii) ipua (iii) baridi (iv) utii (v) lia (vi) tembea (vii) funika (viii) pata (ix) wahi (x)bandika*

D. Kuoanisha maneno na maana zake

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Nakili ubaoni zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 42 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyopo sehemu A na sehemu B. Tumia swali la kwanza na la pili kama mfano.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 42 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) j (ii) f (iii) i (iv) c (v) g (vi) a (vii) e (viii) h (ix) b (x) d*

E. Kuoanisha sehemu A na sehemu B

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu muundo wa insha.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vipengele vya muundo wa insha kwa kutumia insha ya **Maisha ya Kanenge.**

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa 42 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) d (ii) b (iii) c (iv) a*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 38 7/23/21 3:11 PM

Somo la 7: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya na nafasi kati ya neno na neno.

(b) Soma kwa sauti kifungu cha habari kwa kuzingatia alama za uandishi huku wanafunzi wakisikiliza.

> *Siku hizi kuna vijana wakorofi wanaotumia dawa za kulevya, kunywa pombe na kuvuta sigara. Tabia hizo ni mbaya kwa sababu zinawashawishi vijana kujiingiza katika mambo maovu mengi kama vile uhuni, utoro shuleni na ugomvi. Kwa hiyo, wanafunzi msishirikiane na vijana hao. Watawapotosha!*

(c) Soma tena hatua kwa hatua huku wanafunzi wakiandika.

(d) Soma kifungu chote ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hujazisahihisha.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, hati ya wima ya kuunga, matumizi ya herufi kubwa, na usafi wa kazi.

Somo la 8: Ufupisho

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma aya moja.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza aya hiyo kwa maneno machache. Andika maneno hayo ubaoni.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 39 7/23/21 3:11 PM

(d) Waongoze wanafunzi kuunda sentensi kwa kufuata mtiririko wa aya.

(e) Waongoze wanafunzi kulinganisha taarifa zilizopo katika insha ya awali na kile kilichoandikwa kwa maneno machache.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 42 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 9: Utungaji

Kupanga insha kwa kufuata mtiririko mzuri wa matukio kwa kutumia sentensi A – D zilizochanganywa. Kichwa cha habari kiwe "Bibi atembelewa na mjukuu wake"

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(b) Nakili ubaoni kifungu cha habari cha zoezi la 7 kilichopo ukurasa wa 43 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kifungu hicho ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kupanga kifungu hicho kwa mtiririko mzuri kwa mazungumzo.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa 43 katika kitabu cha mwanafunzi.

(f) Sahihisha kazi hiyo kwa kuzingatia hatua za uandishi wa insha, muundo wake uzingatie jina/kichwa cha insha, utangulizi, kiini na hitimisho.

Majibu: *1. B 2. A 3. D 4. C*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 40 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Sita

Kutambua nafsi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza nafsi zote tatu kwa kuzingatia umoja na wingi. Pia, atajifunza namna ya kutumia nafsi hizo katika sentensi au kifungu cha habari. Vilevile, atajifunza misamiati, miundo, nahau, methali, ukanushi, mazoezi mengine ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma habari ya **Sisi na wao**

(b) Kutumia nafsi zote tatu kwa kuzingatia umoja na wingi

(c) Kutumia nafsi katika sentensi fupi

(d) Kutumia nafsi katika kifungu cha habari

(e) Kubainisha silabi zinazoonesha nafsi katika vitenzi

Mahitaji : vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), mazingira halisi, chati za kuonesha nafsi, kadi za maneno, kalamu rashasha na bangokitita

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu swali lililo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 44 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa 45 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 41 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Sisi na wao**, iliyopo katika ukurasa wa 44 - 46 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Nani walikuwa marafiki?

(ii) Nani walishinda mchezo wa kukamata kuku?

(e) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 46 - 47 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri iwezekanavyo.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 42 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *furika, kikongwe, tabasamu, pongezi, totoro, msamaha* na *kisa* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 47 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo namna ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa 47 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mifano iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa 47 katika kitabu cha mwanafunzi namna ya kutumia miundo hiyo katika sentensi.

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na andika sentensi hizo ubaoni.

(f) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 47 katika kitabu cha mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa mfano.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 43 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 4 ukurasa wa 48 katika kitabu cha mwanafunzi. Ongeza mifano mingine.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 ukurasa wa 48 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. si mshindani 2. Samaki mkunje 3. yasiyo na ncha 4. utavuna mabua 5. utengano ni udhaifu*

Somo la 6: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu na maana zake kwa kutumia mfano ufuatao:

Mfano: *fyata ulimi – kaa kimya, nyamaza*
kosa faragha – kutokuwa na siri

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 ukurasa wa 48 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. angusha mtu kwa kutumia miguu 2. panua kinywa huku ukitoa hewa kama ishara ya njaa, uchovu au usingizi 3. saidia mtu 4. chekesha mno 5. kufa au kufariki*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 44 7/23/21 3:11 PM

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari neno linalowakilisha nafsi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya namna ya kutambua maneno yanayoonesha nafsi. Unaweza kutumia chati za kuonesha nafsi na kadi za maneno.

(ii) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa 48 katika kitabu cha mwanafunzi. Ongeza mifano mingine.

Mfano : *Sisi ni wanafunzi wa Darasa la Tano Shule ya Msingi Ngombani.*

Wewe unapenda kusoma?

Ninyi mmefanya vizuri katika mtihani wa Darasa la Nne.

Mimi ninapenda kula wali na nyama ya kuku.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A ukurasa wa 48 - 49 katika kitabu cha mwanafunzi.

B. Kujaza nafsi sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi kwenye sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Toa mifano kwa kujaza nafsi sahihi katika sentensi zifuatazo:

Mfano: ____ *waliondoka jioni.*

Wao waliondoka jioni.

____ *mnaosha vyombo kila Jumamosi.*

Ninyi mnaosha vyombo kila Jumamosi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 45 7/23/21 3:11 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa 49 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i)Mimi* *(ii) Yeye* *(iii) Wao*
(iv) Ninyi *(v) Wewe* *(vi) Sisi*

C. Kukamilisha sentensi kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kukamilisha sentensi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa 49 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa 49 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) a* *(ii) wa* *(iii) ni* *(iv) tu* *(v) u*
(vi) m *(vii) a* *(viii) tu* *(ix) wa* *(x) a*

D. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu mfano uliopo katika zoezi la 6 D ukurasa wa 50 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 D lililopo ukurasa wa 50 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 46 7/23/21 3:11 PM

E. Kuchagua jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia swali la kwanza zoezi la 6 E lililopo ukurasa wa 50 - 51 katika kitabu cha mwanafunzi kama mfano.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 E lililopo ukurasa wa 50 - 51 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) c (ii) d (iii) a (iv) c (v) b (vi) c (vii) d (viii) b*

F. Kubadili sentensi kuwa katika nafsi ya pili wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu nafsi ya pili wingi.

(ii) Toa mfano wa kubadili sentensi kuwa katika nafsi ya pili wingi.

Mfano : *Sisi tulilala mapema jana.*
Ninyi mlilala mapema jana.
Walichelewa kwenda shuleni.
Mlichelewa kwenda shuleni.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 F lililopo ukurasa wa 51 - 52 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo jinsi ya kuandika habari katika mtiririko mzuri.

(b) Nakili mwanzo wa habari ubaoni kutoka ukurasa wa 52 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 47 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma mwanzo wa habari iliyoandikwa ubaoni au katika kitabu cha mwanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kumalizia habari kwa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika zoezi la 7 ukurasa wa 52 katika kitabu cha mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia, matumizi sahihi ya nafsi, mtiririko mzuri, alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 48 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Saba

Wanyama wafugwao

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusimulia hadithi. Pia, atajifunza majina na faida za wanyama wafugwao na vyakula wanavyokula.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma hadithi ya **Kisa cha wanyama kuishi na binadamu**

(b) Kusimulia hadithi

(c) Kutaja majina ya wanyama wafugwao

(d) Kutaja aina za vyakula wanavyokula

(e) Kueleza faida za wanyama wafugwao

Mahitaji: vitu halisi, picha za wanyama wafugwao (za kawaida na za mguso), kalamu rashasha, bangokitita na vikaragosi vya wanyama wafugwao

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 53 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi ya **Kisa cha wanyama kuishi na binadamu** iliyopo katika ukurasa wa 53 - 55 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 49 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali kuhusu habari.

Mfano:

(i) Hapo kale wanyama waliishi wapi?

(ii) Simba alikuwa anashirikiana na wanyama gani?

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie hadithi waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 56 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmoja mmoja kwa zamu bila kujali jinsia na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 50 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *pango, pembe, zizi, samadi* na *kokota* kwa kutumia mbinu ya maelezo, picha na igizodhima.

(b) Andika maneno hayo ubaoni kisha wanafunzi wasome na kueleza maana ya neno mojamoja baada ya majadiliano ya vikundi.

(c) Waongoze wanafunzi wajadili kwenye makundi na kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 56 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile walizofanya katika makundi.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu na maana zake.

(b) Nakili ubaoni zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 57 katika kitabu cha mwanafunzi. Waongoze wanafunzi kusoma nahau zote.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 ukurasa wa 57 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu: *(i) i (ii) g (iii) h (iv) a (v) l (vi) f (vii) e (viii) d (ix) b (x) c*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 51 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Toa mifano na kuiandika ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 57 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *1. moja humponyoka 2. Nazi mbovu 3. humaliza gogo 4. Akufaaye kwa dhiki 5. kiatu chake dawa 6.Udongo uwahi 7. Ukiona vyaelea 8. kuliko fedheha 9. haiui nyoka 10. Kuvuja kwa pakacha*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuorodhesha wanyama wafugwao

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja majina ya wanyama wafugwao wanaowafahamu.

(ii) Andika ubaoni majina ya wanyama wafugwao yaliyotajwa na wanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 58 katika kitabu cha mwanafunzi.

B. Kuchora wanyama wafugwao

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano ubaoni kwa kuchora mnyama mmoja anayefugwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa 58 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 52 7/23/21 3:11 PM

C. Kubadili sentensi ziwe katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Tumia mifano mbalimbali, kwa mfano:

Wanafunzi walikwenda shuleni.
Wanafunzi watakwenda shuleni.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 58 katika kitabu cha mwanafunzi.

D. Kutunga sentensi kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Chora ubaoni jedwali lililopo zoezi la 5 D ukurasa wa 58 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Toa mifano kwa kuandika ubaoni sentensi zifuatazo kutokana na jedwali:

i. Pale kijijini palikuwa na duka kubwa.
ii. Pale nyumbani palikuwa na mti mkubwa.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 58 katika kitabu cha mwanafunzi.

E. Kuandika umoja na wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo mafupi kuhusu umoja na wingi.

(ii) Toa mifano kwa kuandika umoja na wingi.

Mfano :	**Umoja**	**Wingi**
	kiti	*viti*
	chura	*vyura*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 53 7/23/21 3:11 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa 58 - 59 katika kitabu cha mwanafunzi.

F. Kupanga herufi zilizochanganywa ili kupata neno lenye maana sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano kwa kuandika herufi zilizochanganywa ili kupata maneno yenye maana sahihi.

(ii) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 5 F ukurasa 59 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi katika makundi kujadili herufi zilizochanganywa katika zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa 59 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa 59 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu: *(i) tembo (ii) mbuga (iii) twiga (iv) neno (v) ngiri (vi) siku/ kisu (vii) moto (viii) kitabu (ix) mbuzi (x) punda.*

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja mambo ya kuzingatia katika uandishi wa hadithi fupi.

(b) Waongoze wanafunzi kujibu zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 59 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo, na matumizi sahihi ya herufi kubwa. Pia, zingatia faida za mnyama husika na chakula anachokula.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 54 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Nane

Wanyama wa porini

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma na kusimulia hadithi. Pia, atajifunza kuandika hadithi kwa mtiririko sahihi wa matukio. Vilevile, ataweza kutaja majina ya wanyama wa porini na sifa zao.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma hadithi ya **Mkutano wa wanyama**

(b) Kusimulia hadithi

(c) Kutaja majina ya wanyama wa porini

(d) Kutaja sifa za wanyama wa porini

Mahitaji: vitu halisi, picha za wanyama wa porini (za kawaida na za mguso), kalamu rashasha, bangokitita na vikaragosi vya wanyama wa porini

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 60 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi ya **Mkutano wa wanyama**, iliyopo katika ukurasa wa 60 - 62 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 55 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Simba aliunguruma kwa sauti gani?

(ii) Taja vifaa ambavyo wanyama walivitumia kulimia shamba.

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie hadithi waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 63 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsia na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda unavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 56 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *tangatanga, finyanga, shaghalabaghala, msusi, staafu, ning'inia* na *rutuba*. Andika ubaoni misamiati hiyo.

(b) Waongoze kwenye makundi kujadili maana ya maneno hayo.

(c) Waongoze wanafunzi katika makundi kujadili maneno yaliyopo ukurasa wa 63 katika kitabu cha mwanafunzi kwa kutunga sentensi.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 63 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha wanatunga sentensi tofauti na zile zilizotolewa mifano.

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Toa mifano na kuiandika ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 64 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. hunaswa na tundu bovu 2. mauti nyuma 3. Mwenda pole 4. Subira 5. utajenga ukuta 6. ni dhahabu 7. Zimwi likujualo 8. Mchagua jembe 9. aupendao 10. La kuvunda*

Somo la 5: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 57 7/23/21 3:11 PM

Mfano : *kitendawili - tega*

Mjomba hataki tuonane - kisogo

(b) Endapo mwanafunzi hatatoa jibu sahihi, mtegaji apewe mji ili atoe jibu sahihi.

(c) Waongoze wanafunzi kwa kutumia maelezo, picha na mifano kutega na kutegua vitendawili.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 64 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. kivuli 2. chura, samaki, mamba, kiboko 3. pesa, fedha, hela 4. nywele 5. mkonge, nungunungu 6. kinywa 7. machozi 8. nyota 9. siafu.*

Somo la 6: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu na maana zake.

(b) Mifano iliyotajwa na wanafunzi iandikwe ubaoni.

(c) Nakili ubaoni zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 65 katika kitabu cha mwanafunzi. Waongoze wanafunzi kuzisoma nahau zote.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 65 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. fukuzwa kazi 2. kigeugeu 3. tamani 4. toa tangazo 5. kaa tayari au jihadhari 6. kuwa wa mwisho 7. kuongeza maneno yasiyo ya kweli katika taarifa 8. kucheka kwa sauti*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 58 7/23/21 3:11 PM

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kuoanisha maneno yenye maana sawa

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno yenye maana sawa wanayoyafahamu.

(ii) Andika ubaoni mifano miwili au mitatu ya maneno yenye maana sawa.

Mfano : *shaghalabaghala - hovyohovyo*

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa 65 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) h (ii) e (iii) j (iv) i (v) c (vi) g (vii) d (viii) a (ix) f (x) b*

B. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni maneno machache bila kinyume chake.

Mfano : *1. kimbia ……..*
2. wahi ……..

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vinyume vya maneno yaliyoandikwa ubaoni.

(iii) Andika majibu yaliyotajwa na wanafunzi ubaoni.

(iv) Angalia usahihi wa majibu hayo.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa 65 - 66 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *(i) kibaya (ii) karibu (iii) chungu (iv) furaha (v) shangilia (vi) tandua (vii) nunua (viii) fumua (ix) nyamaza (x) achia*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 59 7/23/21 3:11 PM

C. Kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya jinsi ya kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.

(ii) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa 66 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa 66 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) njiwa (ii) uso (iii) nyoka (iv) chupa (v) blanketi (vi) chai (vii) ng'ombe (viii) kaa*

D. Kujaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo kwenye zoezi la 6 D ukurasa wa 66 katika kitabu cha mwanafunzi kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi 6 D lililopo ukurasa wa 66 - 67 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *(i) tetekuwanga (ii) chui (iii) karne (vi) kilele (v) mbuni (vi) yatima (vii) samadari (viii) almasi*

Somo la 8: Ufupisho

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kufupisha habari.

(b) Waongoze wanafunzi kueleza mawazo makuu kutokana na hadithi ya **Mkutano wa wanyama** iliyopo ukurasa wa 60 - 62 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 60 7/23/21 3:11 PM

(c) Andika mawazo hayo ubaoni.

(d) Angalia dosari zilizojitokeza na kuzirekebisha.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa 67 katika kitabu cha mwanafunzi.

(f) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri, na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

Somo la 9: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kusimulia ziara dhahania ya mbuga yoyote ya wanyama kwa kufuata mtiririko wa picha zilizopo ukurasa wa 67 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kuandika hadithi fupi kwa kufuata mtiririko wa picha katika zoezi la 8 lililopo ukurasa wa 67 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 61 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Tisa

Maua

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu majina ya maua, sifa zake, utunzaji na umuhimu wake. Pia, atajifunza misamiati, miundo, methali, imla, ufupisho, utungaji wa shairi na atafanya mazoezi mengine ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma shairi la **Maua**

(b) Kutaja majina na sifa za maua

(c) Kufanya ziara ya kutembelea bustani ya maua

(d) Kueleza umuhimu wa maua

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), bangokitita na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa 68 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu shairi la **Maua** kwa kutumia picha iliyopo ukurasa wa 68 - 70 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi la **Maua** ukurasa 68 - 70 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 62 7/23/21 3:11 PM

(d) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:

(i) Mshairi anasema maua hupatikana wapi?

(ii) Mshairi anasema miti ina utajiri gani?

(e) Waongoze wanafunzi kujibu zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 70 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu kanuni za usomaji wa shairi. Wakumbushe kuwa usomaji sahihi wa shairi huzingatia vina, mizani na kituo.

(b) Soma ubeti wa kwanza kuonyesha mfano mzuri wa usomaji, kwa kuzingatia urari wa vina na mizani.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma shairi mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsia zao na uwezo wao.

(d) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(e) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(f) Wape wanafunzi wengi nafasi ya kusoma kadiri muda unavyoruhusu.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *tunu, fahari, pogolea, ughaibuni, dola, ghasia* na *shamiri*, kwa kutumia maelezo, matendo na vitu halisi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 63 7/23/21 3:11 PM

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo, kisha andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 ukurasa wa 71 katika kitabu cha mwanafunzi. Wanafunzi waandike sentensi tofauti na zile zilizoandikwa ubaoni kama mfano.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu miundo. Rejea katika kipengele cha miundo katika Utangulizi wa kitabu hiki ukurasa wa vi.

(b) Nakili miundo yote ubaoni iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa 71 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo ubaoni na kutoa mifano iliyopo kitabuni.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia mfano wa zoezi la 3 ukurasa 71 katika kitabu cha mwanafunzi, kwa mazungumzo, kisha andika sentensi hizo ubaoni.

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 ukurasa wa 71 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 64 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu methali.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(c) Waongoze wanafunzi kwa kutumia swali la 1 lililopo zoezi la 4 ukurasa wa 71 - 72 katika kitabu cha mwanafunzi kama mfano.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 71 - 72 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1.Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo.*

2. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

3. Akufaaye kwa dhiki, ndiye rafiki wa kweli.

4. Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kutumia herufi zilizochanganywa kuunda maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu uundaji wa maneno kwa kutumia herufi zilizochanganywa.

(ii) Tumia mfano uliopo zoezi la 5 A ukurasa wa 72 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A ukurasa wa 72 - 73 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) mazingira (ii) waridi (iii) vipepeo (iv) asali (v) tunu (vi) dola (vii) wito (vii) wanafunzi (ix) machoni (x) sifa au safi*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 65 7/23/21 3:11 PM

B. Kuandika nyakati katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu viambishi vya nyakati (*_na_, _ li_, _ta_*) katika kitenzi.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa 73 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B ukurasa 73 katika kitabu cha mwanafunzi.

C. Kuandika neno lenye maana sawa na maneno yaliyotolewa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu maneno yenye maana sawa.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 74 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa 74 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) okoa (ii) hongera (iii) jimbi (iv) katani (v) kibonzo (vi) ua/uzio (vii) pori (viii) mwishowe (ix) au (x) shinda/pasi*

D. Kuchagua jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuchagua jibu sahihi kwa kutoa mifano katika zoezi la 5 D lililopo ukurasa 74 katika kitabu cha mwanafunzi

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa 74 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 66 7/23/21 3:11 PM

Majibu : *(i) reli (ii) ugali (iii) ukuli (iv) mkulima (v) maharage (vi) amefaulu (vii) shule zote zitafungwa (viii) rambirambi*

E. Kuandika wingi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuandika sentensi katika wingi kwa kutoa mfano katika zoezi la 5 E lililopo ukurasa 75 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa 75 katika kitabu cha mwanafunzi.

F. Kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na maneno mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ifuatayo kwa kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.

daftari, kalamu, rula, kitabu, *pipi.*

wali, pilau, *mchele*, ubwabwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa 75 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) punda (ii) kunguru (iii) mpira (iv) kanzu (v) gari (vi) ungo (vii) maharage (viii) majigambo*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 67 7/23/21 3:11 PM

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu kanuni na taratibu za utungaji wa shairi linalozingatia urari wa vina na mizani.

(b) Andika ubeti ufuatao ubaoni. Unaweza kutunga ubeti mwingine kwa kuzingatia kanuni zilizotumika kwenye ubeti huu.

Sifa ya mti maua, ishara ya kupevuka,

Chini twajiokotea, mbeguze twanufaika,

Busitanini kusia, na majani hulimbuka,

Nani alitangulia, kati ya mti na ua?

(c) Waongoze kusoma ubeti huu wa shairi, kisha waimbe kishairi.

(d) Waongoze wanafunzi wataje maneno yanayohusiana na maua na kuyaandika ubaoni. Kumbuka maneno hayo yawe na silabi za mwisho zinazofanana.

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye silabi nane kwa kutumia maneno waliyotaja kwa kuzingatia vina. Waeleze kwa kifupi maana ya vina na mizani, pia wakumbushe kuweka mkato kila baada ya silabi nane na mstari wa mwisho kituo (waweke nukta).

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 75 katika kitabu cha mwanafunzi.

(g) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia, alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, matumizi sahihi ya herufi kubwa na urari wa vina na mizani.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 68 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi

Shughuli za kila siku

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atasoma habari kuhusu shughuli za kila siku. Pia, ataeleza shughuli anazofanya nyumbani na shuleni. Vilevile, ataweza kuandika ratiba ya shughuli za kila siku na ataandika habari fupi kwa mpangilio unaoeleweka. Aidha, mwanafunzi atajifunza misamiati, nahau, methali, nyakati na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma habari ya **Chiku anafanya nini kila siku?**

(b) Kueleza shughuli anazotenda nyumbani kwa mpangilio

(c) Kueleza shughuli anazotenda shuleni kwa mpangilio

(d) Kuandika ratiba na habari fupi kwa mpangilio

Mahitaji : vitu halisi, mazingira halisi, picha (za kawaida na mguso), bangokitita, kalamu rashasha, chati ya ratiba ya siku na ratiba ya wiki

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 76 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu habari ya **Chiku anafanya nini kila siku?** ili wapate picha ya jumla.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 69 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Chiku anafanya nini kila siku?** iliyopo ukurasa wa 76 - 78 katika kitabu cha mwanafunzi. Wasisitize wasifuatishe kwa kidole au kutoa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno yao na kueleza funzo walilojifunza.

(e) Waongoze wanafunzi kujibu zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 78 katika kitabu cha mwanafunzi kwa mazungumzo.

(f) Sikiliza majibu ya wanafunzi na rekebisha pale ambapo hawajajibu kwa usahihi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu habari ya **Chiku anafanya nini kila siku?** Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu za kusoma kwa sauti.

(b) Wasomee aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, hisia na matumizi sahihi ya alama za uandishi.

(c) Chagua wahusika wawili; miongoni mwao, awepo mtangazaji na Chiku.

(d) Waongoze wahusika hao kusoma mmojammoja kwa zamu kulingana na uhusika wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo.

(f) Kama kuna makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 70 7/23/21 3:11 PM

(g) Wanafunzi warudie kusoma kwa kubadilishana nafasi za uhusika kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *ratiba, mwagilia, sare, shughuli, tawanyika, wadia* na *usia.*

(b) Andika maneno hayo ubaoni na uwaongoze wanafunzi kusoma maneno hayo.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja na kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Sentensi wanazotunga ziandikwe ubaoni.

(d) Chunguza usahihi wa sentensi walizotunga.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 79 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu.

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo ukurasa wa 79 katika kitabu cha mwanafunzi, kueleza maana ya nahau walizozitaja na kutunga sentensi kwa kutumia nahau hizo.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 79 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. sinzia sana/endekeza usingizi*

2. furahisha moyo/ furahisha mtu sana

3. hisi uchovu/ usingizi/ njaa

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 71 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Kwa kutumia maelezo na mifano, waongoze wanafunzi kutambua maana ya methali.

Mfano: *Harakaharaka haina Baraka - mtu anayefanya jambo kwa pupa na haraka bila utaratibu hafanikiwi katika jambo hilo.*

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 79 - 80 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. b 2. a 3. d 4. b 5. c*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika sentensi katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Waelekeze wanafunzi kuhusu somo hili. Mwanafunzi azingatie silabi '_ta_' inayoonesha wakati ujao katika kitenzi.

(ii) Toa mfano uliopo zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 81 katika kitabu cha mwanafunzi ongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 81 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 72 7/23/21 3:11 PM

B. Kuandika ratiba ya siku

Hatua za ufundishaji

(i) Fafanua kuhusu namna ya kuandika ratiba ya siku kwa kuzingatia shughuli za siku husika.

(ii) Waongoze wanafunzi kuandaa ratiba ya siku ya Jumamosi ambapo huwa wanakuwa nyumbani.

(iii) Waongoze wanafunzi kujadili umuhimu wa ratiba na waelekeze kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa 81 katika kitabu cha mwanafunzi.

C. Kujaza sehemu zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika ratiba.

Mfano:

Siku	***Muda***	***Shughuli***
Jumapili	.....	*Kuandaa sare na vifaa vya shule.*
Jumatatu	*Saa 4:30 asubuhi - saa 5:10 asubuhi*	.....

Siku	***Muda***	***Shughuli***
Jumapili	*Saa 12:00 jioni - saa 1:00 jioni*	*Kuandaa sare na vifaa vya shule.*
Jumatatu	*Saa 4:30 asubuhi - saa 5:10 asubuhi*	*Kuhudhuria kipindi darasani*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 81 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 73 7/23/21 3:11 PM

Majibu:

Siku	***Muda***	***Shughuli***
Jumapili	*Saa 12:00 - saa 1:00 jioni*	***Kuandaa sare na vifaa vya shule***
Jumatatu	*Saa 4:00 - saa 4:30 asubuhi*	***Kupumzika/ mapumziko***
Jumanne	***Saa 8:30 mchana***	*Kutawanyika kutoka shuleni*
Jumatano	***Saa 12:00 jioni***	*Kufungia kuku na mabata bandani*
Alhamisi	*Saa 2:00 asubuhi*	***Kuanza vipindi darasani***
Ijumaa	*Saa 6:30 - saa 6:40 mchana*	***Kupumzika/ mapumziko***
Jumamosi	***Saa 2:00 - saa 3:00 asubuhi***	*Kufua sare za shule*

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujadili hatua za utungaji kwa kutumia picha.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha zilizopo ukurasa wa 82 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusema muda na shughuli inayofanyika kwa kila picha kwa mazungumzo na kuandika maelezo/sentensi hizo ubaoni.

Mfano: *Adamu huamka saa 1:30 asubuhi.*

(d) Andika sentensi hizo ubaoni na kusahihisha makosa yaliyojitokeza.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 82 kwenye kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 74 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Moja

Hali ya hewa

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza mwonekano wa hali ya hewa na aina za hali ya hewa zinazopatikana katika mazingira yake. Pia, atajifunza faida za hali ya hewa katika mazingira yake. Vilevile, atajifunza misamiati, miundo, nahau, methali, ukubwa na udogo wa vitu, umoja na wingi, ukanushi, utungaji na kufanya mazoezi mengine ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma majigambo kuhusu **Hali ya hewa**

(b) Kueleza mwonekano wa hali ya hewa na aina zake

(c) Kueleza faida za hali ya hewa katika mazingira yake

(d) Kutofautisha vitu katika ukubwa na udogo

(e) Kueleza idadi ya vitu vinavyohesabika katika umoja na wingi

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), mazingira halisi, bangokitita na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 83 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu majigambo ya **Hali ya hewa**. Unaweza kutumia picha zilizopo ukurasa wa 83 - 86 katika kitabu cha mwanafunzi. Au tumia picha nyingine ambazo zinaonesha mazingira ya mwonekano wa hali ya hewa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 75 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya majigambo ya **Hali ya hewa** yaliyopo ukurasa wa 83 - 86 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Upepo huweza kupeperusha nini?

(ii) Katika majigambo hayo, methali ya usiandikie mate angali wino upo ina maana gani?

(e) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 87 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri inavyowezekana.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na zisahihishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 76 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *nyesha, madhara, ukame, aghalabu, kasi, vuma, peperusha, umotomoto, fukuto, nyausha, babuka* na *unyevu* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizozitunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 87 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 88 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia nahau wanazozifahamu kwa mazungumzo.

(c) Andika ubaoni sentensi walizotunga wanafunzi.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 88 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 77 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mifano ya majibu ya vitendawili kutega vitendawili.

Mfano: *machozi - maji ya kisima changu hayanyweki.*
chura - hata akioga hatakati.
kivuli - daima hunifuata nyuma, nikimfuata, hunikimbia.

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 88 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: 1. *Nikikutana na adui yangu nanyong'onyea.*
2. Napigwa faini kosa silijui.
3. Kondoo wetu ana nyama nje na ngozi ndani.
4. Ukumbuu wa babu mrefu.
5. Adui tumemzingira lakini hatumwezi.

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kukanusha sentensi kwa kutumia mifano.

Mfano: *Wao ni watoto watukutu.*

Wao si watoto watukutu.

Mjomba anasimulia hadithi vizuri.

Mjomba hasimulii hadithi vizuri.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 78 7/23/21 3:11 PM

(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 88 - 89 katika kitabu cha mwanafunzi.

B. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofanyika.

(ii) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 5 B ukurasa wa 89 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa 89 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) KWELI (ii) SI KWELI (iii) SI KWELI (iv) KWELI (v) SI KWELI (vi) KWELI (vii) SI KWELI (viii) SI KWELI*

C. Kukamilisha sentensi kwa kutumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya namna ya kutumia maneno kutoka kwenye kisanduku ili kukamilisha sentensi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyopo kwenye kisanduku katika zoezi la 5 C lililopo ukurasa 89 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Tumia mfano uliooneshwa katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 89 - 90 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) wengi (ii) mkali (iii) mingi (iv) kubwa (v) kali (vi) mengi (vii) kikubwa (viii) ndogo*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 79 7/23/21 3:11 PM

D. Kubadili sentensi kuwa katika wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu wingi.

(ii) Toa mfano wa kubadili sentensi kuwa katika wingi.

Mfano: *Kijiko kilipotea jana.*
Vijiko vilipotea jana.
Bati limepata kutu.
Mabati yamepata kutu.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 90 katika kitabu cha mwanafunzi.

E. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno na vinyume vyake. Unaweza ukatumia vitenzi kama vile: *kaa - simama, nenda - rudi, cheka - lia, ingia - toka, lala -amka.*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa 90 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) jioni (ii) usiku (iii) dogo (iv) inuka (v) shibe (vi) bondeni (vii) kulia (viii) ibuka au elea (ix) vua (x) hasara*

F. Kutunga sentensi kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili jedwali ubaoni au kwenye bangokitita zoezi la 5 F lililopo ukurasa 91 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kutokana na jedwali hilo kwa kutumia mfano iliyopo katika zoezi la 5 F ukurasa 91 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 80 7/23/21 3:11 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbili kutoka kwenye jedwali kwa mazungumzo.

(iv) Andika ubaoni sentensi zilizotungwa.

(v) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa 91 katika kitabu cha mwanafunzi.

G. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sehemu B

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo jinsi ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sehemu B ili zikubaliane na sehemu A.

(ii) Nakili ubaoni zoezi la 5 G lililopo ukurasa 91 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Tumia swali la kwanza kama mfano.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa 91 katika kitabu cha mwanafunzi.

H. Kutumia herufi za maneno kuunda maneno mapya

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu uundaji wa maneno mengine kutokana na maneno uliyopewa kwa kutumia herufi za maneno hayo.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 H ukurasa wa 92 katika kitabu cha mwanafunzi kuonesha namna ya kuunda maneno mapya. Ongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 H lililopo ukurasa wa 92 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) ziwa (ii) tuta (iii) ita/ tia (iv) wale (v) oza/ zao (vi) mali/ imla/ mila (vii) omba (viii) zua (ix) shiba (x) noa*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 81 7/23/21 3:11 PM

Somo la 7: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya na nafasi kati ya neno na neno.

(b) Soma kwa sauti kifungu cha habari kwa kuzingatia alama za uandishi huku wanafunzi wakisikiliza.

> *Siku ya Jumatatu mvua kubwa ilinyesha kijijini kwetu. Mimi nilichelewa kufika shuleni. Nilipofika shuleni, mwalimu aliniuliza, "Kwa nini umechelewa?" Nikamjibu, "Samahani mwalimu, mvua kubwa ilikuwa inanyesha maeneo ya nyumbani kwetu." Mwalimu akaniruhusu kuingia darasani.*

(c) Soma tena hatua kwa hatua wanafunzi wakiandika.

(d) Soma kifungu chote ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hazijasahihishwa.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, hati ya wima ya kuunga, matumizi ya herufi kubwa, na usafi wa kazi.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu hali ya hewa.

(b) Andika ubaoni mambo ya kuzingatia kama yalivyoandikwa katika zoezi la 6 lililopo ukurasa 92 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa 92 katika kitabu cha mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi ya herufi kubwa. Pia, zingatia lengo la utungaji huo

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 82 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Mbili

Familia yetu

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu maana ya familia na umuhimu wa familia. Pia, atajifunza misamiati, nahau, kinyume cha maneno, umoja na wingi na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma habari kuhusu **Umuhimu wa familia**

(b) Kutaja wahusika katika familia

(c) Kueleza umuhimu wa familia

(d) Kuandika insha kuhusu faida zinazopatikana katika familia

Mahitaji: vitu halisi, picha za familia (za kawaida na za mguso), bangokitita, chati ya muundo wa familia, kalamu rashasha na mti wa familia

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 93 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu habari ya **Umuhimu wa familia.**Tumia picha iliyopo ukurasa wa 95 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Umuhimu wa familia** iliyopo katika ukurasa wa 93 - 95 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 83 7/23/21 3:11 PM

(d) Waulize maswali yafuatayo:

(i) Taja wahusika katika habari hii.

(ii) Eleza tabia ya babu.

(iii) Baada ya miezi mitatu, Doto alifanya nini?

(e) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 95 - 96 katika kitabu cha mwanafunzi kwa kuandika kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu habari itakayosomwa.

(b) Wakumbushe wanafunzi matumizi sahihi ya alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia kanuni sahihi za usomaji.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsia zao na kiwango cha usomaji. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, fuatilia usomaji ili ubaini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda ili kurekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 84 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *mwondoko, makeke, upenuni, madhubuti, kwanyua, amia, taabani* na *churuzika* kwa kutumia maelezo, matendo, mazingira halisi na picha.

(b) Andika maneno hayo ubaoni kisha waongoze wanafunzi kusoma maneno hayo.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 96 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu.

(b) Andika ubaoni nahau zilizopo katika zoezi la 3 ukurasa wa 96 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kuzisoma na kueleza maana zake.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa mazungumzo na uziandike ubaoni.

(e) Waongoze kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 96 katika kitabu cha mwanafunzi. Watunge sentensi nyingine tofauti na zile zilizotolewa mfano.

Majibu: *1. ondoka 2.vumilia 3. moyo safi*
4. kasirisha sana/umiza moyoni 5. kwepa

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 85 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mistari

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya kinyume cha maneno

Mfano: *bandika - bandua*

funga - fungua

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa 96 - 97 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) nyuma (ii) rudi (iii) analia (iv) nimesahau (v) wanachukiana (vi) siyo (vii) alirudi (viii) alikanusha*

B. Kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopita

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya namna ya kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopita ukizingatia kiambishi cha wakati "_li_".

(ii) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopita kwa kutoa mifano.

Mfano: *Mtoto anakunywa uji.*
Mtoto alikunywa uji.
Kisu kitapotea
Kisu kilipotea.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa 97 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 86 7/23/21 3:11 PM

C. Kuandika sentensi katika wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Toa mifano ya kubadili sentensi zilizo katika umoja kuwa katika wingi.

Mfano: *Rafiki yangu amevaa nguo nzuri sana.*

Rafiki zangu wamevaa nguo nzuri sana.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa 97 katika kitabu cha mwanafunzi.

D. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kueleza ukanushi unavyoonekana katika kitenzi.

(ii) Toa mfano wa kubadili sentensi kuwa katika ukanushi.

Mfano: *Tunafurahia kwenda likizo.*

Hatufurahii kwenda likizo.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa 98 katika kitabu cha mwanafunzi.

E. Kuandika sentensi kwa usahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Toa mifano ya sentensi zisizoandikwa kwa usahihi na uwaongoze wanafunzi kuziandika kwa usahihi.

Mfano: *Kitonga ni makao makuu za kiija.*
Kitonga ni makao makuu ya Kiija.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 87 7/23/21 3:11 PM

Mtoto anavisugua sufuria.
Mtoto anasugua sufuria.
Mtoto anaisugua sufuria.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa 98 katika kitabu cha mwanafunzi.

F. Kuandika KWELI au SI KWELI katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa 98 - 99 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: (*i) SI KWELI (ii) KWELI (iii) SI KWELI (iv) SI KWELI (v) KWELI (vi) KWELI (vii) SI KWELI (viii) KWELI (ix) KWELI (x) SI KWELI*

G. Kuchagua neno sahihi kwenye kisanduku ili kukamilisha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutoa mfano wa kukamilisha sentensi. Tumia swali la kwanza katika zoezi la 4 G ukurasa wa 99 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G ukurasa wa 99 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) kuwapongeza (ii) tumeazimia (iii) taji (iv) posta (v) radi (vi) turubai (vii) alitozwa (viii) pancha*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 88 7/23/21 3:11 PM

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(b) Andika maswali ya zoezi la 5 ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali hayo na majibu yake yaandikwe ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 100 katika kitabu cha mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia mtiririko wa mawazo, alama za uandishi, nafasi kati ya neno na neno, uumbaji wa herufi na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 89 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Tatu

Barua rasmi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza jinsi ya kuandika barua rasmi. Atajifunza muundo wa barua rasmi. Pia, ataandika barua rasmi kwa kuzingatia mtiririko wa vipengele vya uandishi wa barua hii. Vilevile, atajifunza misamiati, maana ya methali, ukanushi na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma habari ya **Kabonza amuuguza mama yake**

(b) Kujifunza jinsi ya kuandika barua rasmi

(c) Kueleza muundo wa barua rasmi

(d) Kueleza umuhimu wa barua rasmi

(e) Kuandika barua rasmi

Mahitaji: vitu halisi, chati ya muundo wa barua, bangokitita na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 101 kwenye kitabu cha mwanafunzi.

(b) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu habari ya **Kabonza amuuguza mama yake** iliyopo ukurasa wa 101 - 103 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 90 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari hiyo bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 103 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu habari ya **Kabonza amuuguza mama yake**. Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu sahihi za kusoma kwa sauti.

(b) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, hisia na matumizi sahihi ya alama za uandishi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(d) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(e) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *ugua, sibu, nafuu* na *mwanya* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 91 7/23/21 3:11 PM

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya kila neno.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 103 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazozitunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu zoezi litakalofanyika.

(ii) Toa mifano ya maswali yenye majibu ya KWELI na SI KWELI.

Mfano: *Barua rasmi ina anwani moja. SI KWELI*

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa 104 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) SI KWELI (ii) SI KWELI (iii) SI KWELI (iv) KWELI (v) SI KWELI (vi) SI KWELI*

B. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuandika kinyume cha maneno kwa kutumia mifano.

Mifano: *anika - anua*

tamu - chungu

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 92 7/23/21 3:11 PM

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B ukurasa wa 104 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) pona (ii) pokea (iii) kataza au zuia*
(iv) nukia (v) furahi (vi) laini

C. Kupanga vipengele kwa kufuata muundo wa barua rasmi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu muundo wa barua rasmi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vipengele vya muundo wa barua rasmi katika barua waliyoisoma kwenye habari ya **Kabonza amuuguza mama yake**.

(iii) Waongoze kufanya zoezi la 3 C ukurasa wa 104 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) vii (ii) iv (iii) v (iv) viii (v) ii*
(vi) ix (vii) vi (viii) xi (ix) iii (x) x (xi) i

D. Kujaza muundo wa barua rasmi kwa kutumia vipengele vilivyoomo kwenye kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D ukurasa wa 105 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 93 7/23/21 3:11 PM

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waandikie wanafunzi ubaoni mambo ya kuzingatia kama yalivyoandikwa katika zoezi la 4 ukurasa wa 105 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili mambo yaliyoandikwa ubaoni.

(c) Andika ubaoni majibu yaliyojadiliwa.

(d) Angalia usahihi wa majibu yaliyoandikwa.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 ukurasa wa 105 katika kitabu cha mwanafunzi.

(f) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, matumizi sahihi ya herufi kubwa, na kuzingatia mtiririko wa vipengele vya uandishi wa barua rasmi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 94 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Nne

Igizo

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza namna ya kusoma igizo na kuliigiza. Pia, ataeleza wazo kuu na fundisho katika igizo hilo. Vilevile, atajifunza matumizi ya nafsi na nyakati katika kauli halisi na kauli taarifa, kisha atafanya mazoezi mengine ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma igizo linaloitwa **Maskini Tukutu**

(b) Kueleza maudhui yaliyomo katika igizo na kuchambua wazo kuu

(c) Kuigiza

(d) Kubadili sentensi katika kauli halisi na kauli taarifa

(e) Kutambua matumizi sahihi ya nafsi na nyakati katika sentensi

Mahitaji: vitu halisi, mazingira halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati, bangokitita, diski ya igizo (sidii ya igizo), projekta, televisheni, deki, kinyonyi na kompyuta

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 106 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo katika ukurasa wa 106 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 95 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya igizo linaloitwa **Maskini Tukutu**, ukurasa wa 106 – 109 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kusimulia igizo walilolisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 ukurasa wa 109 katika kitabu cha mwanafunzi. Waongoze kufanya swali la 1 - 4 kwa mazungumzo na swali la 5 - 8 kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu sahihi za kusoma kwa sauti.

(b) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia. Zingatia usomaji wa majibizano kwa kubadili sauti kwa kila mhusika.

(c) Chagua wanafunzi wasome kwa kuzingatia wahusika wote waliopo kwenye igizo.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 96 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Kazi ya kufanya (Igizo)

Hatua za ufundishaji

(a) Teua wahusika kwa kuzingatia wahusika waliopo kwenye igizo.

(b) Toa maelekezo kwa wahusika.

(c) Wape muda wahusika kujiandaa na kuwasilisha kazi yao (igizo).

(d) Fanya hitimisho la igizo na wapongeze kwa kufanya vizuri.

Somo la 4: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *igizo, mtukutu, mbinja, nyang'anya, kwida* na *kaidi* kwa kutumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo kisha andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 ukurasa wa 110 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazozitunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu kwa kutaja mianzo au miisho na wengine kukamilisha na kusema maana zake.

(b) Angalia usahihi wa miisho na mianzo ya methali walizozitaja wanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 97 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 110 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. Mtu anayekufaa au kukusaidia wakati wa shida ndiye rafiki wa kweli.*

2. Kwa kawaida mtoto hukua jinsi anavyolelewa. Akilelewa vibaya, ataishia kuwa na tabia mbaya.

3. Kitu kilichozoeleka huwa ni kama kanuni.

4. Ukitaka kupata manufaa, wafuate watu watakaokusaidia kupata manufaa hayo.

5. Usibaki katika tatizo wakati uwezo wa kujitoa katika tatizo hilo upo.

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika maneno yenye maana sawa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

Mfano: *tisa - kenda*
mwanzo - awali

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 110 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu : *(i) yowe (ii) nenda (iii) mluzi (iv) mtundu / mgomvi/ mkorofi, (v) tele / nyingi sana/ tumbi (vi) pora (vii) kaba*

B. Kubadili sentensi kutoka umoja kwenda kwenye wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu namna ya kubadili sentensi za umoja kuwa katika wingi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 98 7/23/21 3:11 PM

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 B ukurasa wa 111 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa 111 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

C. Kutunga sentensi kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo katika zoezi la 5 C ukurasa wa 111 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyopo kwenye jedwali.

(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi tano kama mfano.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 111 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

D. Kubadili sentensi kuwa katika kauli taarifa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya jumla kuhusu namna ya kubadili sentensi kuwa katika kauli taarifa.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 D ukurasa wa 111 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 111 katika kitabu cha mwanafunzi.

E. Kujaza fumbo kwa kutumia maelezo ya kwenda chini na kwenda kulia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 99 7/23/21 3:11 PM

(ii) Nakili fumbo na maelekezo ya kwenda chini na kulia ubaoni au kwenye bangokitita kama yalivyo katika zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa 112 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Toa mfano wa kwenda chini wa swali la kwanza kwa kuuliza swali lifuatalo: 1. Kifaa kinachotumika kulalia (herufi 7) - KITANDA.

(iv) Andika jibu hilo kwenye vyumba kuanzia namba 1 kwenda chini. Kila chumba kiandikwe herufi moja.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa 112 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

			1 K		2 K	I	T	A	B	U
		3 V	I	N	A					
			T		L			4 M		
5 D	A	R	A	S	A			A		
			N		6 M	W	I	K	O	
			D		U			T		
			A					A		
								B		
								A		

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 100 7/23/21 3:11 PM

F. Kuchagua jibu sahihi na kisha kuliandika katika kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa 113 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *(i) a (ii) b (iii) a (iv) c (v) b*

G. Kuunda maneno mapya

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu namna ya kuunda maneno mapya kwa njia ya mwambatano wa maneno.

(ii) Tumia mfano uliopo zoezi la 5 G katika ukurasa wa 114 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G ukurasa wa 114 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) askarikanzu (ii) batamzinga (iii) garimoshi (iv) mwendokasi (v) zimamoto (vi) pimajoto/pimamaji (vii) pembetatu/ pembenne/ pembezoni (viii) maliasili/ malighafi (ix) kandambili*

H. Kukamilisha jedwali kwa kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopo na ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo.

(ii) Nakili ubaoni jedwali lililopo zoezi la 5 H ukurasa wa 114 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 101 7/23/21 3:11 PM

(iii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi mojamoja katika jedwali.

(iv) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopo na ujao kwa kutumia mifano ifuatayo:

Mfano : *Mimi ni**na**maliza kazi zote kabla ya kwenda kulala. (uliopo)*

*Mimi ni**ta**maliza kazi zote kabla ya kwenda kulala. (ujao)*

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 H ukurasa wa 114 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya somo.

(b) Andika ubaoni mwanzo wa hadithi kama ilivyoandikwa katika zoezi la 6 ukurasa wa 114 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma mwanzo huo.

(d) Waongoze wanafunzi kumalizia hadithi kwa kuzingatia mwanzo uliopo katika zoezi la 6 ukurasa wa 114 katika kitabu cha mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na herufi kubwa. Zingatia usahihi wa matumizi ya nafsi na nyakati.

(f) Baada ya kusahihisha, chagua hadithi iliyoandikwa vizuri na wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 102 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Tano

Shairi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu mashairi. Ataweza kuonesha na kueleza dhana ya vina, mizani, beti, vituo, na mawazo makuu kwenye mashairi hayo.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kujifunza kuhusu mashairi

(b) Kusoma na kuimba/kughani mashairi

(c) Kueleza maana ya shairi

(d) Kueleza vina, mizani, mshororo na ubeti

(e) Kueleza mawazo makuu na ujumbe katika shairi

Mahitaji : vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), shairi la mfano, manila na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 115 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi la **Yai au kuku** lililopo ukurasa wa 115 - 117 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(c) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:

(i) Shairi linahusu nini?

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 103 7/23/21 3:11 PM

(ii) Shairi lina beti ngapi?

(iii) Shairi lina sifa nyingine unayoitambua?

(iv) Unapenda nini kuhusu shairi hili?

(d) Waongoze wanafunzi kueleza kwa kifupi kuhusu shairi la **Yai au kuku** na kueleza funzo walilojifunza.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 117 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji sahihi wa shairi kwa kuzingatia kiimbo na hisia kwa kutumia ubeti mmoja wa shairi au zaidi.

(b) Wakumbushe wanafunzi maana na idadi ya mizani katika kila mstari kwa kuonesha na kuhesabu mizani hiyo.

(c) Wafundishe maana ya vina na jinsi ya kuvitambua. Vina ni silabi zinazolingana katikati na mwishoni mwa ubeti wa shairi. Wakati mwingine shairi huwa na ulingano wa vina mwishoni mwa ubeti tu. Mstari wa ubeti unaitwa mshororo.

(d) Waongoze wanafunzi kutaja vina vya kati na vya mwisho.

(e) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kila ubeti kwa zamu bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(f) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(g) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na kurekebisha makosa hayo.

(h) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 104 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *pekua, ibukia, tembe, piku, zogo, bongo, chapuchapu, mzozo, jadi, sulubu, rai, komaa na miongo.* Tumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 ukurasa wa 118 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotumika kama mifano wakati wa somo.

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Rejelea ufundishaji wa methali katika sehemu ya utangulizi ukurasa wa vii katika kitabu hiki.

(b) Toa mifano ya kukamilisha methali, kama ifuatavyo:

(i) Chovyachovya …….
Chovyachovya <u>humaliza buyu la asali.</u>

(ii) ..... *haiui nyoka.*
<u>Fimbo ya mbali</u> haiui nyoka.

Mwalimu chagua wanafunzi wa kumalizia methali hizi.

(c) Wape nafasi wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 118 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 105 7/23/21 3:11 PM

Majibu: *1. yai lake au yaile* *2. halimuumizi mwanawe*
3. hakosi kamba mguuni *4. hafunzwi kuchakura*
5. aujuaye mzazi

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuchagua jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalolifundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa 119 - 120 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) (d) (ii) (c) (iii)(a) (iv)(a) (v) (c) (vi) (c) (vii) (c) (viii)(d)*

B. Kuandika kwa ukamilifu maneno yaliyofupishwa katika shairi

Hatua za kufundishia

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalolifundisha.

(ii) Toa mifano ya ufupisho unaowezekana, kwa mfano:

jinale – jina lake

mamangu – mama yangu

dadangu – dada yangu

nilompa – niliyempa

(iii) Waongoze kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa 121 wa kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) sura yake (ii) aliibukia (iii) umepata wapi (iv) akili zako*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 106 7/23/21 3:11 PM

C. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuandika kinyume cha maneno.

Mifano: *nyeupe – nyeusi*

ndefu – fupi

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C kuhusu kinyume ukurasa wa 121 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) jibu (ii) giza (iii) mwisho (iv) ongeza (v) kifo/mauti (vi) kwamua (vii) kumbuka (viii) heshimu (ix) tegua (x) chache*

D. Kuandika neno lenye maana sawa na neno lililotolewa

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuandika maneno yenye maana sawa na maneno yaliyotolewa.

Mifano : *tazama – angalia*

haraka – upesi

dunia – ulimwengu

katu – kamwe

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa 121 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) shinda/ pita/ zidi (ii) beza/ tweza (iii) vutia/ furahisha*

(iv) enda mbele (v) uhai (vi) feli (vii) ruhusa (viii) tamko

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 107 7/23/21 3:11 PM

Somo la 6: Utungaji

Kutunga beti mbili za shairi kuhusu ‘Kifaranga na kuku’

Hatua za Ufundishaji

(a) Toa mfano wa shairi kwa wanafunzi kwa kutumia shairi lenye ubeti mmoja au zaidi kidogo.

(b) Shairi lisomwe na liimbwe.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma na kuimba mstari kwa mstari. Kila mstari una idadi ya silabi 16, na nusu mstari una silabi 8. Hizi huitwa mizani. Waongoze katika kuhesabu mizani hizo.

(d) Waelekeze wanafunzi kuwa katika kila ubeti zipo silabi zinazolingana kwa jinsi zinavyotamkwa na kuandikwa, katikati na mwishoni mwa mstari. Silabi hizi huitwa vina.

(e) Waongoze kutaja vina vya kati na vya mwisho katika kila ubeti.

(f) Waeleze wanafunzi kuwa kila mstari katika ubeti huitwa mshororo.

(g) Waeleze wanafunzi kuwa mstari wa mwisho katika ubeti huitwa kituo.

(h) Waongoze wanafunzi kuzungumzia zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 121 katika kitabu cha mwanafunzi.

(i) Andika ubaoni kila wazo linalotolewa na wanafunzi kuhusu mada ya zoezi.

(j) Waongoze wayapange maneno yote kwa utaratibu wa ulingano wa silabi za mwisho wa maneno, yaani utaratibu wa urari wa vina.

(k) Waongoze kutunga ubeti mmoja wa mfano kwa kutumia maneno hayo na mengine.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 108 7/23/21 3:11 PM

(l) Waelekeze wanakili ubeti uliouandika ubaoni kwa mpangilio sahihi.

(m) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5, lililopo ukurasa wa 121 katika kitabu cha mwanafunzi.

(n) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia matumizi sahihi ya alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na herufi kubwa.

(o) Chagua mashairi mawili ambayo yameandikwa vizuri yasomwe darasani.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 109 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Sita

Kuipenda nchi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi ataimba **wimbo wa kuisifu nchi yetu,** kisha atasoma na kughani shairi la **Naipenda nchi yangu**. Mwanafunzi atajifunza habari mbalimbali kuhusu nchi yetu, kama vile maziwa makubwa, mlima maarufu wa Kilimanjaro, mito, lugha ya Kiswahili, na mambo mengine. Ataweza pia kuonesha na kueleza vina, mizani, beti, vituo, na mawazo makuu katika shairi.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kuimba **Wimbo wa kuisifu nchi yetu**

(b) Kusoma na kuimba shairi la **Naipenda nchi yangu**

(c) Kueleza dhana ya vina, mizani, mshororo na ubeti

(d) Kueleza habari muhimu katika wimbo na shairi

Mahitaji : vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), shairi la mfano, manila na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kuimba wimbo wa kuisifu nchi yetu kwenye kipengele cha *fikiri* katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo ukurasa wa 123 kwenye kipengele cha *fikiri* katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 110 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi la '**Naipenda Nchi Yangu**' lililopo ukurasa wa 123 - 128 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(d) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza la ufahamu lililopo ukurasa wa 128 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Soma ubeti mmoja au beti mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, na hisia sahihi katika usomaji wa mashairi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(d) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(e) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(f) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

(g) Waongoze wanafunzi kuimba shairi mmojammoja kwa zamu. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kuimba.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 111 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *neema, maumbile, miinuko, bonde, tambarare, kilele, vijito, hodhi, ghaidhi, wigo, tumbitumbi, sanaa, hadhi, nuia* na *murua*. Tumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi zilizotungwa na wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 129 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kuoanisha maneno ya sehemu A na maana zake katika sehemu B

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mifano ya maneno yaliyopo katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.

Mfano:

Sehemu A	Sehemu B
tambarare	*ardhi isiyo na miinuko wala mabonde*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 112 7/23/21 3:11 PM

Katika mfano huu, maana ya **tambarare** imeoneshwa katika safu ya sehemu B.

(ii) Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A ukurasa wa 129 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) f (ii) d (iii) a (iv) e (v) b (vi) i (vii) h (viii) g*

B. Kuandika sentensi zilizotolewa katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu zoezi litakalofanyika.

(ii) Toa mfano uliotolewa katika zoezi la 3 B ukurasa 130 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi hilo.

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu kanuni na taratibu za utungaji wa shairi linalozingatia urari (yaani, ulinganifu) wa vina na mizani, lenye beti za mistari/ mishororo minne minne.

(b) Andika ubeti uliochagua kuutumia kama mfano. Tumia mfano huu ukikosa mwingine:

Kata yetu ya Runzewe, ni kata bora twajua,

Ni makini katibuwe, hutenda kwa kujitoa,

Wote hasa wakaziwe, juhudi huzingatia,

Naisifu kata yangu, kata yangu ya Runzewe.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 113 7/23/21 3:11 PM

(c) Wasomee wanafunzi ubeti wa shairi. Kama unaweza, uwaimbie au umchague mwanafunzi mmoja aimbe.

(d) Waongoze wanafunzi kutaja sifa mbalimbali zinazohusiana na **darasa lao.** Hakikisha sifa nyingi zinatajwa iwezekanavyo huku ukiziandika ubaoni.

(e) Waongoze wanafunzi kupanga maneno yanayoonesha sifa za darasa lao (na mengine yanayoambatana nayo) kufuata miisho inayolingana (yaani, urari wa vina), kwa mfano : *elimu, karimu, nidhamu; tabia, zingatia, kujitoa, murua; shirikiana, saidiana, fanana, tegemeana* na mengineyo.

(f) Waongoze wanafunzi kutunga mistari yenye silabi nane kwa kutumia maneno waliyotaja kwa kuzingatia vina. Waeleze kwa kifupi maana ya vina na mizani. Pia, wakumbushe kuweka mkato kila baada ya silabi nane na katika mstari wa mwisho (kituo) waweke mkato kulingana na mahitaji.

(g) Waongoze wanafunzi kutunga ubeti kwa pamoja, kuanzia mstari wa kwanza hadi wa nne, kwa kuwauliza : *Tuanze na neno lipi ? neno lipi lifuate? na kadhalika.*

(h) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 130 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha beti zitakazoandikwa na wanafunzi zisifanane na mifano ya darasani.

(i) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, urari wa vina na mizani, na mtiririko mzuri wa shairi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 114 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Saba

Utenzi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu utenzi. Ataweza kuonesha na kueleza vina, mizani, beti, kituo na mawazo makuu kwenye utenzi huo.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kujifunza kuhusu utenzi

(b) Kusoma na kuimba utenzi

(c) Kueleza maana ya utenzi

(d) Kueleza vina, mizani, mshororo na ubeti katika utenzi

(e) Kueleza mawazo makuu na ujumbe katika utenzi

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), mfano wa utenzi, manila na kalamu rashasha

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri***,** ukurasa wa 131 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya utenzi wa **Usafi** uliopo ukurasa wa 131 - 133 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 115 7/23/21 3:11 PM

(c) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:

(i) Utenzi huu unahusu nini ?

(ii) Una beti ngapi ?

(iii) Utenzi huu unafananaje au unatofautianaje na tenzi ulizowahi kuzisoma ?

(iv) Unapenda nini katika utenzi huu?

(d) Waongoze wanafunzi kueleza kwa kifupi kuhusu utenzi juu ya **Usafi,** kisha waeleze funzo walilolipata.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 133 - 134 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji sahihi wa utenzi kwa kuzingatia kiimbo na hisia kwa kutumia ubeti mmoja wa utenzi au zaidi.

(b) Wakumbushe wanafunzi maana na idadi ya mizani katika kila mstari wa ubeti kwa kuonesha na kuhesabu mizani hiyo.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza utaratibu wa vina katika utenzi huu.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma ubeti kwa zamu kila mmoja bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 116 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *zingatia, kinga, zonga, longa, staftahi, saki, sukutua, auni, kutuzi, nadhifu* na *kunjufu.* Tumia mbinu ya maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 134 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazozitunga hazifanani na zile zilizotolewa kama mifano.

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Rejelea ufundishaji wa methali katika sehemu ya utangulizi, ukurasa wa vii katika kitabu hiki.

(b) Toa mifano ya kukamilisha methali, kama ifuatavyo:

Aliye kando .....

Aliye kando <u>haangukiwi mti.</u>

.....ni deni.

<u>Ahadi</u> ni deni.

Chagua wanafunzi wa kumalizia methali hizi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 117 7/23/21 3:11 PM

(c) Wape nafasi wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 134 - 135 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *1. hayana pazia 2. hayaumani 3. kuliko meno 4. hapotei 5. hauna mfupa 6. Baada ya dhiki 7. Ndondondo 8. Usipoziba ufa 9. Tamaa mbele 10. La kuvunda*

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu na maana zake, kwa mfano:

Nahau	**Maana**
kuona cha mtema kuni	*kupata mateso au matatizo mazito*
kiinua mgongo	*malipo ya uzeeni*

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa 135 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. kuwa kigeugeu*

2. fuata mawazo ya wakati uliopo

3. kuwa na wasiwasi

4. kaa kimya

5. kujitia matatani/ kujiweka kwenye matatizo

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 118 7/23/21 3:11 PM

Somo la 6: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu

Mfano: Kitendawili – tega

Anatembeza ndevu zake lakini hapati mnunuzi - Mahindi

Endapo mwanafunzi hatatoa jibu sahihi, mtegaji apewe mji ili atoe jibu sahihi.

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 135 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu : *1. kamasi 2. macho 3. chunguchungu*
4. kiberiti 5. jani la mti / tunda

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kukamilisha sentensi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa 136 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) mwanafunzi (ii) ukiwa (iii) anarina (iv) tasa*
(v) naam / abee (vi) mchafu (vii) maziwa (viii) njuga
(ix) kwaheri (x) sonara

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 119 7/23/21 3:11 PM

B. Kuandika umoja au wingi wa maneno yaliyotolewa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Toa mifano ya umoja na wingi, kwa mfano *jina – majina , mti – miti, kalamu – kalamu.*

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa 136 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 8: Utungaji

Kutunga beti mbili za utenzi kuhusu usafi wa nyumba

Hatua za ufundishaji

(a) Toa mfano wa utenzi kwa wanafunzi kwa kutumia utenzi wenye beti mbili au zaidi kidogo.

(b) Utenzi usomwe na uimbwe.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma na kuimba mstari kwa mstari. Kila mstari una idadi ya silabi 8. Silabi hizi huitwa mizani. Waongoze katika kuhesabu mizani hizo.

(d) Waelekeze wanafunzi kuwa, katika ubeti mwishoni mwa kila mstari, zipo silabi zinazofanana au zinazolingana kwa jinsi zinavyotamkwa na kuandikwa. Silabi hizi huitwa vina.

(e) Waongoze kutaja vina katika kila ubeti.

(f) Waelekeze wanafunzi kuwa mstari wa mwisho katika ubeti huitwa kituo.

(g) Waongoze wanafunzi kuzungumzia zoezi la 7 ukurasa wa 136 katika kitabu cha mwanafunzi. Wanafunzi wataje maneno na mafungu ya maneno yanayohusiana na **Usafi wa Nyumba.**

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 120 7/23/21 3:11 PM

(h) Andika ubaoni kila neno au fungu linalotolewa na wanafunzi kuhusu mada husika.

(i) Waongoze wanafunzi kupanga maneno yote kwa utaratibu wa ulingano wa silabi za mwisho wa maneno, yaani utaratibu wa urari au ulinganifu wa vina.

(j) Waongoze wanafunzi kutunga ubeti mmoja wa mfano kwa kutumia maneno hayo na mengine.

(k) Waelekeze wanafunzi kunakili ubeti uliouandika ubaoni kwa mpangilio sahihi.

(l) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa 136 katika kitabu cha mwanafunzi.

(m) Sahihisha kazi za wanafunzi, kwa kuzingatia kanuni za uandishi wa utenzi. Chagua tenzi mbili au tatu ambazo zimeandikwa vizuri. Zisomwe na kuimbwa darasani.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 121 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Nane

Kupata taarifa muhimu

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma na kueleza taarifa muhimu kutokana na matangazo, ratiba, na vifungu vya habari mbalimbali. Pia, atataja mawazo makuu na kufanya ufupisho wa vifungu vya habari. Vilevile, atajifunza misamiati, miundo, nahau, methali, utungaji na mazoezi mengine ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma tangazo, ratiba, na vifungu vya habari

(b) Kueleza taarifa muhimu kutokana na matangazo, ratiba, na vifungu vya habari

(c) Kutaja mawazo makuu kutokana na vifungu vya habari

(d) Kufanya ufupisho wa vifungu vya habari

Mahitaji: ratiba, picha (za kawaida na za mguso), chati ya matangazo mbalimbali, kalamu rashasha na bangokitita

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* kwenye ukurasa wa 137 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Nia na mdogo wake** iliyopo katika ukurasa wa 137 - 140 bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 122 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
   (i) Bute na Nia walisoma katika shule gani?
   (ii) Nani alipotea?
   (iii) Nani aliandaa tangazo?

(d) Wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache, kisha waeleze taarifa mahususi walizozipata.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 140 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili za habari ya **Nia na mdogo wake** kuonesha mfano mzuri wa usomaji, kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, hisia na matumizi sahihi ya alama za uandishi.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 123 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *hema, shtuka, nakala, lowa, hofu, pongeza, himiza* na *ghafla.*

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kuyasoma.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja na kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 lililopo ukurasa wa 141 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *i. (c) ii. (e) iii. (b) iv. (h) v. (i) vi. (d) vii. (a) viii. (f)*

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa 141 katika kitabu cha mwanafunzi na uwaongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo.

(c) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 3 ukurasa wa 141 katika kitabu cha mwanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia muundo huo kwa mazungumzo na uandike sentensi hizo ubaoni bila kujali usahihi wake.

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi. Rekebisha zenye dosari.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 124 7/23/21 3:11 PM

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 141 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Toa mifano michache kuhusu namna ya kutumia nahau katika sentensi. Mifano hiyo itokane na nahau zilizotumika katika habari ya **Nia na mdogo wake** iliyopo ukurasa wa 137 – 140 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Nakili ubaoni zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa 142 katika kitabu cha mwanafunzi kisha waongoze wanafunzi kusoma nahau zote.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana za nahau hizo kwa kuzungumza, kisha andika ubaoni maana zake.

(d) Angalia usahihi wa maana hizo.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A na B lililopo ukurasa wa 142 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 6: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Rejea ufundishaji wa methali katika sehemu ya Utangulizi ukurasa wa vii katika kitabu hiki.

(b) Toa mifano michache ya kukamilisha methali.

Mfano : *Mtoto umleavyo,……*
Mtoto umleavyo, <u>ndivyo akuavyo.</u>

Ukiona vyaelea, ……
Ukiona vyaelea, <u>vimeundwa.</u>

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 125 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(d) Angalia usahihi wa methali zilizotajwa na wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 142 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. hayazoleki 2. pana njia 3. hulia kivulini 4. haiozi 5. hujaza kibaba*

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano michache ya maneno na vinyume vyake.

Mfano: *juu - chini*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa 142 – 143 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) pangua (ii) chini (iii) fungua (iv) zima (v) dogo (vi) mwembamba (vii) vuta (viii) meza (ix) fukua (x) pakua*

B. Kuandika umoja na wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Andika mifano michache ubaoni.

Mfano: Umoja	**Wingi**
shamba	*mashamba*
nyumba	*nyumba*
kinu	*vinu*

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa 143 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 126 7/23/21 3:11 PM

Somo la 8: Utungaji

A. Kuandika habari fupi kuhusu shughuli za nyumbani. Zingatia muda wa kufanya shughuli hizo

Hatua za ufundishaji

(i) Ongoza mazungumzo kuhusu shughuli zinazofanywa na wanafunzi wakiwa nyumbani kwa kuzingatia muda wa shughuli hizo.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 A lililopo ukurasa wa 143 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi ya herufi kubwa.

B. Kuandaa tangazo fupi

Hatua za ufundishaji

(i) Ongoza mazungumzo kuhusu siku za mitihani ya Darasa la Nne iliyofanyika mwaka uliopita kwa kuuliza maswali kama:

Mtihani ulianza siku gani na tarehe ngapi?

Wanafunzi walifanya mitihani hiyo wakiwa wapi?

Je, wanafunzi wa madarasa mengine walihudhuria shuleni?

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 B lililopo ukurasa wa 143 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao kwa kuzingatia vipengele vilivyotajwa.

(iii) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, taarifa muhimu katika tangazo na matumizi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 127 7/23/21 3:11 PM

Somo la 9: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kusoma kimya kifungu cha habari kilichopo katika ukurasa wa 144 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.

(b) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Kwa nini Sheku alisikitika sana?

(ii) Nani alimsomesha Sheku?

(c) Wanafunzi wasimulie habari kwa maneno machache na waeleze wazo kuu kutokana na kifungu hicho.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 8 lililopo ukurasa wa 144 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 10: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu kifungu cha habari walichosoma kimya katika ukurasa wa 144 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.

(c) Soma sentensi mbili au tatu za kifungu cha habari ili kuonesha mfano mzuri wa usomaji, kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, hisia, na matumizi sahihi ya alama za uandishi.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsia zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 128 7/23/21 3:11 PM

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na zisahihishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na kurekebisha makosa hayo.

Somo la 11: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *azimia, wahenga, nia,* na *sikitika*.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kuyasoma.

(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja na kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 9 lililopo ukurasa wa 145 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 12: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 10 ukurasa 145 katika kitabu cha mwanafunzi na waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo.

(b) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 10 ukurasa wa 145 katika kitabu cha mwanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na uandike sentensi hizo ubaoni bila kujali usahihi wake.

(c) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi. Rekebisha sentensi zenye dosari.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 129 7/23/21 3:11 PM

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 10 lililopo ukurasa wa 145 katika kitabu cha mwanafunzi. Hakikisha wanafunzi hawarudii sentensi zilizotolewa mifano.

Somo la 13: Mazoezi ya lugha

A. Kubadili sentensi kuwa katika uyakinishi:

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu uyakinishi.

(ii) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi za ukanushi kuwa yakinishi. Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 11 A lililopo ukurasa wa 145 katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 11 A lililopo ukurasa wa 145 - 146 katika kitabu cha mwanafunzi.

B. Kubadili vitendo kuwa majina

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 11 B ukurasa 146 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 11 B lililopo ukurasa wa 146 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) mlinzi (ii) mkulima (iii) mfugaji (iv) msomaji au msomi (v) mchoraji (vi) mjenzi/ jengo (vii) tamko (viii) msako*

C. Kuandika sentensi katika wakati uliopita

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo jinsi ya kuandika sentensi katika wakati uliopita kwa kuzingatia silabi ya wakati '**_li_**' katika kitenzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 130 7/23/21 3:11 PM

(ii) Toa mfano uliopo katika zoezi la 11 C ukurasa wa 146 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 11 C lililopo ukurasa wa 146 - 147 katika kitabu cha mwanafunzi.

D. Kuandika maneno sahihi kutokana na herufi zilizochanganywa

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 11 D ukurasa wa 147 katika kitabu cha mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 11 D lililopo ukurasa wa 147 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) sherehe (ii) ubao (iii) mpira (iv)asante (v) zoezi (vi) ratiba (vii) tangazo (viii) yangu (ix) jambo (ix) kipepeo*

Somo la 14: Ufupisho

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu taratibu za ufupishaji wa habari.

(b) Waongoze wanafunzi kueleza mawazo makuu kutokana na kifungu cha habari kilichopo ukurasa wa 137 - 140 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Andika mawazo yao ubaoni bila kujali usahihi wake.

(d) Angalia dosari zilizojitokeza na kuzisahihisha.

(e) Waongoze wanafunzi kufupisha kifungu cha habari kilichopo ukurasa wa 137 - 140 katika kitabu cha mwanafunzi kwa kuzungumza.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 12 lililopo ukurasa wa 147 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 131 7/23/21 3:11 PM

(g) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo, na matumizi ya herufi kubwa.

Somo la 15: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Ongoza mazungumzo kuhusu somo la utungaji.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mada ya utungaji kama ilivyobainishwa katika zoezi la 13 lililopo ukurasa wa 147 katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuwaongoza kwa kuuliza maswali yafuatayo:

(i) Unalipenda somo gani?

(ii) Linafundishwa na mwalimu nani?

(iii) Kwa nini unalipenda?

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 13 lililopo ukurasa wa 147 katika kitabu cha mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 132 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Kumi na Tisa

Sifa za wanyama

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu wanyama wanaokula majani na wanyama wanaokula nyama kutokana na majigambo yao. Pia, atajifunza sifa na faida za wanyama hao. Vilevile, atajifunza misamiati, miundo, utungaji na mazoezi mbalimbali ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma majigambo kuhusu wanyama

(b) Kueleza sifa za wanyama

(c) Kutaja faida za wanyama

(d) Kuigiza majigambo ya wanyama

Mahitaji: kalamu rashasha, bangokitita, picha (za kawaida na za mguso), chati ya wanyama na vikaragosi

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri,* ukurasa wa 148 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya majigambo ya wanyama katika ukurasa wa 148 - 155 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kidole na bila kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 133 7/23/21 3:11 PM

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo kwa kuzungumza:

(i) Kati ya wanyama wote waliojigamba ni mnyama yupi ana meno makubwa?

(ii) Kwa nini twiga anatembea kwa madaha?

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 lililopo ukurasa wa 155 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.

(c) Chagua wanafunzi kumi (10) ambao watavaa uhusika wa wanyama wanaojigamba katika majigambo.

(d) Waongoze wanafunzi kuigiza majigambo kwa kusoma kwa sauti.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Waongoze wanafunzi waigize majigambo kwa kusoma kwa sauti kwa kubadilishana kadiri muda utakavyoruhusu.

Somo la 3: Msamiati

A. Kuoanisha maneno ya sehemu A na sehemu B kwa kuandika jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Fundisha misamiati ifuatayo: *mapato, thamani, mbuga, watalii, samadi, madaha, sumu, sufu, milia, mithili* na *tanga.*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 134 7/23/21 3:11 PM

(ii) Andika maneno hayo ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kuyasoma.

(iii) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja na kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(iv) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 A lililopo ukurasa wa 156 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) f (ii) j (iii) h (iv) n (v) d (vi) e (vii) b (viii) a (ix) g (x) k (xi) i*

B. Kutunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyotolewa

Hatua za ufundishaji

(i) Fundisha misamiati ifuatayo: *mashuhuri, cheua, ngurumo, buruta, rarua, sufu, thamani, madaha, samadi* na *machonge.*

(ii) Andika maneno hayo ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kuyasoma.

(iii) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja.

(iv) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 2 B ukurasa wa 157 katika kitabu cha mwanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo.

(v) Andika sentensi hizo ubaoni.

(vi) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 B lililopo ukurasa wa 157 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 135 7/23/21 3:11 PM

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Nakili miundo yote ubaoni iliyopo katika zoezi la 3 katika ukurasa wa 157 katika kitabu cha mwanafunzi na waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo.

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 3 kwenye ukurasa wa 157 katika kitabu cha mwanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo, kisha andika sentensi hizo ubaoni bila kujali usahihi wake.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi, kisha rekebisha sentensi zenye dosari.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 157 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofanyika.

(ii) Toa mifano michache yenye majibu ya KWELI na SI KWELI

Mfano: *Mwezi wa tisa huitwa mwezi Septemba.* <u>*KWELI*</u>

Mwezi wa saba huitwa mwezi Juni. <u>*SI KWELI*</u>

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa 158 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 136 7/23/21 3:11 PM

B. Kuandika majina kumi (10) ya wanyama kwa kutumia herufi zilizomo kwenye jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Chora jedwali lililopo katika zoezi la 4 B ukurasa wa 158 katika kitabu cha mwanafunzi ubaoni au kwenye bangokitita.

(ii) Toa mfano mmoja uliotiwa kivuli ukurasa wa 158 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa 158 - 159 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: Majina ya wanyama wanaokula nyama: *paka, chui, mbwa, simba, fisi*

Majina ya wanyama wanaokula majani wanaweza kuwa: *kiboko, kobe, punda, tembo, swala, mbuzi, ngamia, farasi.*

C. Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya wanyama

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyomo kwenye kisanduku katika zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa 159 katika kitabu cha mwanafunzi.

(iii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa 159 katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa 159 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 137 7/23/21 3:11 PM

D. Kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano michache kwa kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.

Mfano: kunguru, mwewe, kuku, paka, bata, njiwa

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa 159 katika kitabu cha mwanafunzi.

E. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano michache ya maneno na kinyume chake.

Mfano: *nenda - rudi*

chomeka - chomoa

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa 159 - 160 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu : *(i) mwaga (ii) fichua (iii) fumbua (iv) gumu*
(v) fumua (vi) kunjua (vii) nyooka (viii) tenganisha

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Andika ubaoni vipengele vya kuzingatia katika utungaji kama vilivyoorodheshwa katika zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 160 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili vipengele hivyo kimoja baada ya kingine kadiri muda utakavyoruhusu. Andika majibu ubaoni.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 138 7/23/21 3:11 PM

(c) Angalia usahihi wa majibu yaliyoandikwa ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga habari fupi kwa kuzingatia vipengele vilivyobainishwa katika zoezi la 5 lililopo ukurasa wa 160 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, matumizi ya herufi kubwa, mtiririko wa matukio, na maudhui ya habari husika.

(f) Baada ya kusahihisha, chagua habari iliyoandikwa vizuri, kisha wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 139 7/23/21 3:11 PM

Sura ya Ishirini

Miti yetu

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu aina mbalimbali za miti. Pia, atajifunza faida na umuhimu wa miti. Vilevile, atajifunza misamiati, nahau, methali, uundaji wa maneno, utungaji na mazoezi mbalimbali ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) Kusoma habari kuhusu **Msitu wa Mzee Sunga na mazimwi**

(b) Kutaja aina mbalimbali za miti

(c) Kueleza faida na umuhimu wa miti

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya methali, bangokitita, kalamu rashasha, chati ya nahau na chati ya alama za uandishi

Somo la 1: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu swali lililopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa 161 katika kitabu cha mwanafunzi.

(b) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu habari ya **Msitu wa Mzee Sunga na mazimwi**. Tumia picha iliyopo katika ukurasa wa 162 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Msitu wa Mzee Sunga na mazimwi** iliyopo katika ukurasa wa 161 - 164 katika kitabu cha mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 140 7/23/21 3:11 PM

(d) Waulize maswali yafuatayo:

(i) Mazimwi yaliyotajwa katika habari ni mangapi?

(ii) Taja vitu vinavyopatikana msituni.

(iii) Asali hutengenezwa na mdudu gani?

(e) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 1 la ufahamu lililopo ukurasa wa 165 katika kitabu cha mwanafunzi.

Somo la 2: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu habari itakayosomwa.

(b) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili ili kuonesha mfano mzuri wa usomaji, kwa kuzingatia kanuni sahihi za usomaji.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsia zao na kiwango chao cha usomaji. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, fuatilia usomaji ili ubaini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda ili kurekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 141 7/23/21 3:11 PM

Somo la 3: Msamiati

A. Kutunga sentensi moja kwa kila neno ulilopewa

Hatua za ufundishaji

(i) Fundisha misamiati ifuatayo: *mchakacho, kokwa, ada, tokomea, hirizi, taharuki, shawishi, dadisi, murua, pango, rasilimali* na *rithi* kwa kutumia maelezo, matendo, mazingira halisi na picha.

(ii) Andika maneno hayo ubaoni na wanafunzi wayasome.

(iii) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja.

(iv) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(v) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi, kisha watunge sentensi nyingine kwa kuandika.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 A lililopo ukurasa wa 165 katika kitabu cha mwanafunzi. Wasirudie sentensi zilizotungwa wakati wa somo.

B. Kuoanisha maneno ya sehemu A na maana zake katika sehemu B

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano wa kuoanisha maneno ya sehemu A na sehemu B ili kueleza maana.

Mfano:

Sehemu A	**Sehemu B**
adhimu	c. enye ubora wa pekee

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 2 B lililopo ukurasa wa 166 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) c (ii) d (iii) a (iv) e (v) b*

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 142 7/23/21 3:11 PM

Somo la 4: Nahau

Kutunga sentensi mbili kwa kila nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu.

(b) Andika ubaoni nahau zilizopo zoezi la 3 kwenye ukurasa wa 166 katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma nahau na kueleza maana zake.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi na ziandike ubaoni.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa 166 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. kutokata tamaa 2. kaa tayari 3. bahili/ mchoyo*
4. lia kwa sauti kubwa 5. kuwa na maringo/ kujivuna

Somo la 5: Methali

Kukamilisha methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 ukurasa wa 166 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *1. halikuli likakwisha 2. Kidole kimoja 3. hulia kivulini*
4. Baniani mbaya 5. kibaya chajitembeza

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 143 7/23/21 3:11 PM

Somo la 6: Mazoezi ya Lugha

A. Kuandika maneno yenye maana sawa na maneno yaliyotolewa

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuandika maneno yenye maana sawa na maneno waliyopewa. Tumia mfano ufuatao:

msitu - pori

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa 166 - 167 katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu: *(i) kua/ pendeza (ii) ruhusa (iii) tamani/ vutiwa (iv) zuru (v) fanicha (vi) hifadhi (vii) buruta (viii) panda (ix) chana (x) ondoka/potea*

B. Kuandika neno moja badala ya kikundi cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusiana na somo litakalofundishwa.

(ii) Toa mfano wa kundi la maneno na kuandika neno moja linalowakilisha kundi hilo.

Mfano: *sahani, kikombe, kijiko, bakuli - <u>vyombo</u>*

iliki, mdalasini,karafuu, vitunguu saumu - <u>viungo</u>

(iii) Waongoze wanafunzi kujibu swali la 5 B lililopo ukurasa wa 167 katika kitabu cha mwanafunzi.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 144 7/23/21 3:11 PM

Majibu: *(i) miti (ii) samani (iii) wadudu (iv) wanyama*
(v) matunda (vi) nafaka (vii) nguo/mavazi (viii) silaha

C. Kuandika KWELI au SI KWELI katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutoa mfano wa sentensi ya kujibu KWELI au SI KWELI

Mfano: *Mpingo unafaa kutengenezea vinyago - KWELI*

Mazimwi huishi na binadamu - *SI KWELI*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa 167 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) KWELI (ii) KWELI (iii) SI KWELI (iv) SI KWELI*
(v) KWELI (vi) KWELI (vii) KWELI (viii) SI KWELI

D. Kuchagua jibu sahihi na kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Mfano: *Kalamu _____ imevunjika.(langu, changu, yangu)*
Kalamu <u>yangu</u> imevunjika.
Mtoto _____hajafika. (wako, lako, chako)
Mtoto <u>wako</u> hajafika.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 145 7/23/21 3:11 PM

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa 168 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) wangu (ii) yake (iii) lake (iv) chake (v) vyao (vi) wetu (vii) zake (viii) yetu*

E. Kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza katika nafasi zilizoachwa wazi.

Mfano: *Mtu anayefanya kazi ya kufundisha ni _____*
(mwalimu, daktari, mwanasheria)
Mtu anayefanya kazi ya kufundisha ni <u>mwalimu</u>.

Mtu anayefanya kazi ya kupika chakula ni _____
(mwimbaji, mpishi, mvuvi).
Mtu anayepika chakula ni <u>mpishi.</u>

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa 168 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu: *(i) mtego (ii) fundi seremala (iii) nahodha (iv) rubani (v) Mkwezi (vi) mesenja (vii) mfinyanzi (viii) reki*

F. Kupanga herufi zilizochanganywa ili kupata majina ya miti

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano wa kupanga herufi za neno zilizochanganywa ili kupata neno lenye maana.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 146 7/23/21 3:11 PM

Mfano: *metob* - *tembo*

koshe - *kesho*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa 169 katika kitabu cha mwanafunzi.

Majibu:

(i) mvule (ii) mkoko (iii) mbuyu (iv) mpingo
(v) mninga (vi) mkungu (vii) mlonge (viii) mvinje

Somo la 7: Ufupisho

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(b) Waongoze wanafunzi kueleza kwa kifupi habari waliyoisoma kwa mazungumzo.

(c) Waongoze wanafunzi kulinganisha taarifa zilizopo katika habari iliyofupishwa na kifungu cha habari cha awali.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa 169 katika kitabu cha mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia mtiririko wa hoja, matumizi ya alama za uandishi, nafasi kati ya neno na neno, uumbaji wa herufi, na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 147 7/23/21 3:11 PM

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Waongoze wanafunzi kupata majibu ya vidokezo vilivyopo ukurasa wa 169 katika kitabu cha mwanafunzi kwa mazungumzo. Majibu yaandikwe ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kuunganisha mawazo hayo ili kuandika habari fupi kwenye madaftari yao.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia mtiririko wa hoja, alama za uandishi, nafasi kati ya neno na neno, uumbaji wa herufi, na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KISWAHILI KIONGOZI LEO KILICHODOGOSHWA22.indd 148 7/23/21 3:11 PM